# ***MTAMAUKO***

***Alex Barasa***

© **Alex Barasa,** 2023

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu ya kitabu hiki inayoweza kunaswa tena au kusambazwa kwa namna yoyote au kwa njia yoyote ile, kielektroniki au kimakanika, ikijumuisha kunakili, kurekodi, au kwa mfumo wowote wa kuhifadhi na kurejesha taarifa, bila kibali cha maandishi cha mchapishaji, isipokuwa pale inaporuhusiwa na sheria.

**ISBN-17: 979-8862-64-187-5**

Imechapishwa na Kuchapishwa na Elong'o Publishers

Nairobi, Kenya

Barua pepe: info@elongopublishers.co.ke

Simu: +254742433826

Tovuti: https://elongopublishers.co.ke

# *Tabaruku*

Shukrani za dhati toka katika kipembe cha moyo wangu zikammiminikie babangu mzazi Pius Barasa na mama zangu Eunice Namalwa, Caroline Nakhumicha na Jackline Rupia. Katika usanjari huu pia namshukuru amu yangu Michael Chepkenda ambaye pia alinifanikishia masomo yangu. Nyie ni shujaa. Malezi yenu hayana badala yake. Baba na amu mliniusia nisome na hakika sikukaidi ushauri wenu. Nilisoma na ninaendelea kusoma.

# Yaliyomo


Tabaruku ........ iii

Sura ya kwanza ........ 2

Sura ya pili ........ 8

Sura ya tatu ........ 14

Sura ya nne ........ 18

Sura ya tano ........ 23

Sura ya sita ........ 29

Sura Ya Saba ........ 32

Sura Ya Nane ........ 40

Sura Ya Tisa ........ 43

Sura Ya Kumi ........ 48

Sura Ya Kumi na Moja ........ 53

Sura Ya Kumi na Mbili ........ 59

Sura ya kumi na tatu ........ 69

Sherehe ........ 73

# *Sura ya kwanza*

"Muhibu wangu Fatuma, hivi wajua kwamba mwanamke na mwanamume ni malaika walioumbwa kupaa pamoja? Kati ya wanawake wote duniani niliowahi kukutana nao mimi nimekuchagua wewe. Nimechagua kupaa nawe kama malaika mwenza. Uzuri na urembo wako wenye mvuto hauna badala yake popote pale duniani." Nikatanguliza. "Wewe nawe utaniua kwa maneno yako haya yaliyo matamu zaidi ya uki!" Fatuma akajibu huku akitabasamu kwa tabasamu yake yenye mnato. Aghalabu kila alipotabasamu urembo na uzuri wake uliongezeka maradufu. Vidu vilivyojitokeza mashavuni kila alipotabasamu, macho yake ya gololi, nyusi nyeusi tititi, nywele zake za kipilipili na mdomo wake wa kasiba vyote vilichanga bia kumzidishia urembo wake wa kuitikisa dunia.

"Kukurambisha asali toka moja kwa moja kwenye sega la nyuki ni jukumu langu mie. Mpenzi wangu Fatuma ninakumithilisha na chemchemi yenye maji maenge iliyochipuka ghafla jangwani mbele ya mtu aliyekuwa anaelekea kufa kutokana na kiu ya maji. Ninakupenda sana mpenzi wangu Fatuma. Ninatamani sana n'kafanikiwe nikakutimizie haja zako zote. Ninaamini ipo siku." Nikaendelea kumfurahisha Fatuma kwa nyama ya ulimi. Fatuma alilifurahia kila tamko toka kinywani mwangu huku akiyarembua macho yake.

Tulipokuwa tukiendelea na mazungumzo yetu humo chumbani huku tukicheka kwa furaha tele zilizotutawala, tulisikia mbisho mlangoni. Baada ya kunyanyuka pale kochini na kuufungua mlango, nilikutana uso kwa uso na mmiliki wa nyumba hiyo tulimoishi pale mlangoni. Hata bila salamu alianza kunifokea, "Mwezi wa pili ndio huu sasa ushaanza ila bado hamjalipa kodi ya nyumba! Si nyie wasomi tena wenye mishahara mikubwa mikubwa? Sasa nawapa siku mbili tu, endapo hamtakuwa mmelipa kodi nitawafurusha toka katika nyumba yangu hii!" Baada ya

kusema kwa ghadhabu aliondoka. Ujio wake mlangoni petu ulidhihirisha uchovu wa kusubiri aliokuwa nao. Alikuwa amechoshwa na kuchushwa na ahadi zangu hizo za mara kwa mara ambazo alihisi kwamba hazitimiziki. Je, lakini ilikuwa kupenda kwangu kweli kutomtimizia ahadi yangu hiyo; ahadi ya kulipa kodi ya chumba hicho nilimoishi mimi na mke wangu Fatuma? La hasha! Haikuwa kwa ridhaa yangu kabisa. Ni hali ya ***ukalili*** wa hela ndiyo iliyonilazimu. Maneno yake yaliyosheheni ghadhabu na vitisho yakanizamisha katika bahari ya luja. Nikawaza na kuwazua kuhusu hali hiyo ya ***ukata*** iliyotuandama kwa siku ayami kama kivuli.

Niliiwazia elimu ya nchini kwetu ambayo baada ya kuhitimu hususan mafunzo ya vyuo mtu anafaa kuajiriwa kulingana na taaluma aliyoisomea nikaishia kuinunia na kuichukia. Elimu niliyohisi kuwa imemea mkono wa birika ikaninyima matunda yake. Lakini elimu kweli? Labda ilikuwa ni serikali ya nchi yangu ndiyo iliyoninyima matunda ya elimu; yaani kutonipa ajira. Naam! Ilikuwa serikali na mfumo wake wa uongozi wa kutopanua nafasi za kazi kwa vijana.

Tajiri au maskini ambaye hakuhudhuria hata masomo ya chekechea angemuonaje msomi fukara? Angeionaje au angeichukulia vipi elimu? Si angeishia kuidharau elimu tu bila kutambua kwamba elimu ndio uti wa mgongo katika kila nyanja? Je, yumkini nchi yetu ndiyo haikuchangamkia suala la ajira kwa waliohitimu masomo yao ya vyuoni? Iweje mtu aliyehitimu masomo ya chuo aondokee kuwa ***mchuuzi*** mjini huku akijinyenyekeza kwa watu wanunue bidhaa zake huku wale waliokosa kwenda shule wakiendesha ***mashangingi*** na hata kuwatifulia wasomi vumbi barabarani? Haiwezekani na haifai kabisa! Kwamba wote waliokwenda shuleni na wale hawakwenda wana haki ya ***kunafasika*** kulingana na bidii ya mtu binafsi pamoja na utumizi wake wa akili, pia wasomi na elimu yao wanafaa kupewa ***hadhi*** yao. Wasomi wanafaa kuhongerwa kwa kuajiriwa pindi wanapohitimu masomo yao. Waone na

kuyafurahia matunda ya bidii yao katika elimu ili waweze kujikwamua toka katika minyororo ya dhihaka, masimango na dharau za ***wakwasi*** na ***wakata*** ambao hawakwenda skulini.

Mara ghafla niligutushwa toka katika mawazo hayo mazito mle chumbani mwangu kwa mguso wa mkono laini begani. Ulikuwa mguso nilioufahamu barabara. Mguso wa mchumba wangu Fatuma. Fatuma kasimama nyuma yangu hali amefadhaika zaidi. "Mume wangu! Mawazo yatakumaliza wewe! Usiwaze sana." Fatuma alisema. "Lakini hadi lini tutaendelea kuabiri kwa mtumbwi huu wa uhawinde? Kama ni vyeti na maarifa vyote tunavyo. Wewe hapo ulipo ni mhasibu, unacho cheti chako halali kabisa baada ya kufuzu nami hapa nilipo ni mhandisi. Tena mwenye cheti halali kabisa baada ya kufuzu. Kama ni kazi tumetafuta sana. Kwa siku nyingi tumekuwa kiguu na njia kubisha hodi katika afisi mbali mbali za serikali kuomba kazi ila hatujafua dafu.

Ni mwongo mmoja sasa umepita tukiwa tunasaka kazi bila mafanikio. Yumkini kuna mja ametupoka sudi yetu? Tumeomba kazi hata katika mashirika ya kibinafsi ila juhudi zetu zimekuwa tasa. Watu wanaajiriwa kwa kujuana na kwa kupeana rushwa. Cha kutamausha zaidi ni kwamba kuna wale walioajiriwa kwa kughushi au kutumia uwezo wao wa kifedha kununua vyeti. Sisi wenye vyeti *original* na halali kabisa tumewachwa nje. Kamwe hatuthaminiwi kabisa pamoja na juhudi zetu na maarifa mengi. Sisi maskini ambao hatuna *connections* hatuna letu kabisa! Eti siku hizi lazima uwe na watu wako walio na ushawishi serikalini ndio usaidike." Nilisema kwa ghadhabu. "Hali itaimarika tu, jana si leo na leo si kesho. *Yesterday is not today and today is not tomorrow. Each day rises fresh from the hands of 'Were' to bring whatsoever it will* alisema *Margaret. A Ogola* katika kitabu chake *The River and The Source.* Inawezekana kuna mwanga kesho mpenzi wangu," Fatuma alinitia moyo. "Lakini mchumba wangu Fatuma, hivi unajua kwamba unampa mgonjwa ***malana*** tumaini la

kupona ilhali mwenyewe tayari ameshaliona kaburi lake?" Nikamjibu Fatuma kwa mfadhaiko.

Abadani sikuona matunda ya mahangaiko ya muda mrefu shuleni. Uwepo wangu shuleni kuanzia darasa la chekechea hadi chuo kikuu nilikumithilisha na kupoteza muda wangu tu kuhangaikia jambo lisilo na hata tone la tija. Laiti kungediriki kunionjesha hata tone la tija yake niwe na matumaini madhali nilisadiki kwamba matumaini humpa mtu moyo wa kujaribu tena. Wavyele wetu waliojisabilia na ***kujifunga masombo*** hali ***wanajikusuru*** watulipie ada ya shule wangejivunia nini? Binafsi matamanio yangu yalikuwa kwamba nibahatike kuajiriwa nikawafae wazazi wangu kwa kunisomesha. Sikutaka kabisa ije itokee habari ya kufanikiwa na kisha kuwatamausha kwa ***kuwatelekeza*** wazazi wangu. Huko kungekuwa sawa na fadhila za punda ambazo daima ni... Abadani sikutaka niwalipe mateke kwa fadhila zao za kupigiwa mfano.

Maskini kila nilipoenda usaili nilinyimwa nafasi hiyo ya ajira kwa madai kwamba sikuwa na tajriba wala uzoefu. Nilishindwa jinsi ningepata tajriba hiyo au uzoefu huo madhali hakuna yeyote aliyenipa kazi ili nipate tajriba hiyo. Wote walitaka tajriba kabla ya kunipa kazi. Hapo ndipo msingi imara wa kuwachukia mno wasaili wenye hulka ya kutanguliza tajriba kama moja wapo ya vigezo muhimu ya kuajiriwa ulipojengeka moyoni mwangu. Hivi, utamtarajia vipi mtu ambaye hajawahi ajiriwa kazi awe na tajriba? Kwa mtazamo wangu mtu kama huyo anafaa aajiriwe ili aweze kupata tajriba na wala si kunyimwa kazi kwa kutoafikia kigezo hiki. Siku zote nilihisi kwamba wasaili hususan waliokwisha lishwa milungura walitumia sababu hiyo kuninyima kazi.

"Muhibu, naona bora nijaribu kwenda Uarabuni. Inawezekana riziki yangu ipo kule. Inawezekana nikapata '*green pasture*' huko, yaani mapato makubwa kule. Wewe waonaje mke wangu?" Nilimpendekezea Fatuma wazo langu. "Wazo hilo zuri ila ukienda utaniwacha na nani? Je,

kule utakwenda vipi ikiwa kodi ya nyumba pekee yatutoa jasho? Hiyo nauli utaimudu kweli mume wangu?" Fatuma aliuliza kwa mfuatano. Maswali yake yalinitafakarisha na kunifikirisha mno. Ikabidi niwaze kwa kitambo kirefu kabla ya kumjibu, chambilecho wahenga ni bora kuenga kabla ya kujenga. "Nitaenda kuzungumza na wazazi nyumbani wanisaidie kupata nauli ili nifanikishe safari hiyo. Wewe napendekeza kwamba utaenda nyumbani kwetu ukakae na wakwe zako huku ukiendelea kutuma maombi ya kazi. Ujaribu tu huenda ***nyota ya jaha*** ikakushukia." "Lakini kazi yenyewe tumekwishaitafuta sasa huu ni mwaka wa kumi bila mafanikio! Imekuwa sawa na kutarajia kupata sindano katika nyazi ndefu gizani. Mimi naona bora twende wote." Fatuma alisema na kupendekeza kwa mfadhaiko.

"Kwenda sote si hoja. Hoja ni nauli za kutufanikishia usafiri wetu sote tutazitoa wapi? Isitoshe, kule ndio ninaenda kusaka kazi yenyewe si kwamba nina uhakika kwamba kazi hiyo ipo yanisubiri. Wacha mimi nizungumze na wazazi wanisaidie nisafiri. Nikifika huko na kupata ajira nitakuwa nikikutumia hela za matumizi. Aidha, nikifanikiwa kuyalainisha mambu yangu, nitakushughulikia nawe uje. Sawa mke wangu?" Nilimjibu Fatuma na kisha kumuuliza endapo aliafikiana nami huku akiwa ametulia kifuani pangu nami nikimgusagusa taratibu mgongoni. Fatuma bila kutamka lolote akatikisa kichwa, ishara ya kukubaliana nami ijapokuwa shingo upande. Hatukuwa na njia nyingine mbadala ila kukubaliana kwa mapendekezo hayo. Nilikuwa mbuzi ambaye singeendelea kula kwa urefu huo wa kamba yangu. Urefu ambao abadani haungenitosha. Nilihisi kwamba kamba yangu hiyo ilikuwa fupi mno. Njia pekee ya ya kujiongezea shibe ilikuwa ni kuikata ili nijitimizie haja na ndoto zangu.

Hatimaye nilibahatika kufanikisha safari yangu hiyo ya kwenda Uarabuni kusaka kazi. Nilipania kufanya kazi yoyote ile ipatikanayo huko. Waama mwenye njaa hachagui chakula kilicho tamu au kile ambacho si

kitamu. Chochote kijacho mbele yake yeye yu tayari kukifakamia kama fisi mwenye njaa ya juma nzima muradi chashibisha na kuitokomeza njaa. Fatuma alinisindikiza hadi katika uwanja wa ndege na kabla ya kupanda kwenye ndege tuliagana kwanza na kutakiana heri. Katika kuagana huko nilimpiga Fatuma pambaja nikahisi jinsi moyo wake ulivyodunda. Machozi nayo yalimchirizika kama maji yamwagikayo toka kwenye ***bilula***. Nadhani hisia za uchungu wa utengano huo zilikuwa ***zimemuelemea.*** Fatuma aliponiambukiza hisia hizo nami machozi yakaanza kunidondoka bila kutarajia. Nikauona na kuuhisi upendo wa dhati uliokuwepo kati yetu. Ama kweli kutengana kuna tabu. "Muhibu ingawa kimwili tunatengana bado moyoni tuko pamoja na daima tutasalia kuwa pamoja. Ninaahidi kukutunzia penzi lako nawe tafadhali nitunzie langu!" Nilimwambia na kumrai Fatuma kabla ya kuingia kwenye ndege.

# *Sura ya pili*

Nilipoingia ndani ya ndege, zilikuwa zimebakia dakika chache tu ndege hiyo iweze kung'oa nanga toka katika uwanja huo wa kimataifa wa *Vijiweni*. Ndege yenyewe iliitwa *Hawinde Airways*. Ilikuwa ni ndege yenye ukubwa wa wastani. Ilikuwa bado alfajiri mbichi kabisa ambapo anga lililokuwa limetawaliwa na utusi utusi mwanzoni sasa lilikuwa limeanza kuwa na uchechea. Baada ya kuketi kwenye kiti nilichotengewa mle ndegeni, nilitunduia nje kupitia kwenye dirisha la ndege lililokuwa karibu nami. Pale nikaliona jukwaa la kupungia wasafiri mikono likiwa limejaa sisisi watu waliofika katika uwanja huo kuja kuwaaga wendani wao. Nikamtazama Fatuma naye akanitazama kwa huruma na kite. Tukapungiana mikono ya kwaheri kwa mara ya mwisho kwa takriban dakika tatu hivi.

Kwa kawaida machozi ya mwanamume huja kwa ***tukizi*** mno kama mvua jangwani. Wakati huo machozi yalinitiririka bila kutarajia. Msemo wa baadhi ya watu kwamba machozi usoni pa mwanamume hayastahili kabisa madhali yameumbiwa makoo tu na wala si majogoo kamwe haukunizuia kuzidhihirisha hisia zangu katika hali hiyo iliyonikabili na kuniandama kama nzi kwenye kinyesi. Sikutaka kutengana na Fatuma kabisa. Nilitamani ningekuwa na uwezo tusafiri wote ila sikuwa na uwezo huo. Aidha, nikawazia kukatisha safari hiyo ila nilipofikiri jinsi maisha yalivyoniwia magumu nikaghairi nia. Nikaona bora niende tu. Niende nikasake maisha katika bara lingine hilo ambalo sikuwa nimewahi kukanyaga mguu wangu kwalo tangu kuzaliwa kwangu. Hiyo ilikuwa mara yangu ya kwanza kabisa kuabiri kwa ndege maishani mwangu.

Hata ndege ilipoanza kwenda, nilikuwa bado napungiana mikono hiyo ya kwaheri na Fatuma. Sote tulisononeka zaidi kwa utengano huo ambao hatukuufanya kwa ridhaa yetu wenyewe bali kutokana na hali ngumu ya

maisha. Si kwa kawaida chochote kinachobanwa na kukandamizwa hujaribu kufurukuta ili angalau kijinusuru? Sikuwa na budi kufurukuta ili nijinasue toka kwenye mkatale huo wa ukata uliokuwa unaelekea kutunyanyasa na kutukandamiza zaidi. Fatuma alikuwa bado kanitungia macho kwa jitimai. Niliufunika uso wangu ulioshamiri mavune kwa vitanga vyangu na kisha kuyafuta machozi yaliyokuwa karibu yanipofushe kwa hanchifu niliyokuwa nayo.

Ilikuwa desturi yangu kusali kila mwanzoni mwa safari yoyote ile ili nikamtangulize Rabana katika safari yangu. Akaniepushie mipango mibaya ya ibilisi. Hivyo basi niliinamisha kichwa changu ***nikapiga bismilahi*** kwake Karima. Hiyo ilikuwa mara yangu ya kwanza kabisa kuabiri kwa ndege maishani mwangu. Nilipomaliza na kisha kuinua kichwa changu, katika mkono wangu wa kushoto nilimuona binti mmoja aliyekuwa ameketi karibu nami kanikazia macho sana. Nikaamua kumuamkua, " Dada hujambo?" "Sijambo mie kakangu. Habari za kwako?" Yule binti alijibu na kisha kuendeleza salamu. "Njema tu nashukuru dada," nikamjibu. "Mimi naitwa Neema. Wewe je?" Akajitambulisha na kisha akauliza. "Mimi jina langu ni Yohana." Nikamjibu.

Mazungumzo kati yangu na Neema yakaendelea kadri tulivyoendelea na safari yetu hiyo ya angani. Awali tuliendelea na utambulisho. Kila mmoja akajitambulisha kwa mwenziwe kwa kina. Nilipigwa na butwaa nilipobaini kuwa niliwahi kusoma na Neema kuanzia darasa la chekechea hadi darasa la tatu katika moja kati ya shule za msingi zilizopatikana kijijini kwetu Msonge. Shule yenyewe iliitwa *Angaza*. Kama nilivyomfahamu enzi hizo, hakuwa wa kujumlisha moja na moja akapata kumi na moja bali mbili tena kwa wepesi na haraka zaidi.

Kuibuka nambari moja katika kila mtihani tulioufanya wa mara kwa mara ndio uliokuwa desturi yake Neema. Aliwahi kuwa nambari mbili

mara moja tu baada ya mimi ***kumpiku*** na kuja katika nafasi yake hiyo katika moja kati ya mitihani tuliyowahi kufanya. Nakumbuka alighadhabika zaidi nilipomshinda katika mtihani huo. Mamake alikuwa mwalimu aliyetufundisha katika shule hiyo ya msingi ya Angaza. Kwa bahati mbaya mamake huyo na babake baadaye walihusika katika ajali mbaya ya barabarani wakaaga dunia. Wakamwacha Neema mikononi mwa nyanyake na babu yake ambao baadaye walimhamisha toka katika shule hiyo ya msingi ya *Angaza* na kumpeleka katika shule nyingine ambayo sikuwahi ifahamu. Hapo ndipo tulipoondoana machoni hadi tulipokutana siku hiyo katika safari hiyo ya ndege. Babu na nyanyake ***walijisabilia*** kumsomesha hadi akahitimu masomo ya chuo kikuu kulingana na alivyonieleza katika mazungumzo hayo.

Neema alikuwa ametaalumia uhasibu kama mke wangu Fatuma. Naye alikuwa yuaelekea Uarabuni kusaka kazi yoyote ambayo angeipata kule. Katika mazungumzo hayo niligundua kuwa mimi na Neema tuliabiri mtumbwi mmoja. Mtumbwi wenye madhila si haba kutokana na kutopata ajira nchini kwetu hata baada ya mahangaiko ya muda mrefu ya kuisaka. Naye alikuwa amekata shauri. Shauri la kwenda katika bara hilo lingine kusaka kazi hata kama kule tungekumbana na tatizo la kubaguliwa. Pana ajabu gani nzi kufia kidondani? Tulikuwa radhi kukabiliana na vyovyote vile viwavyo kule.

"Yohana mimi naudhika sana kuona jinsi serikali ya nchi yetu haijaipa kipaumbele ajira kwa wanaohitimu masomo yao. Yasikitisha mno kuona mtu aliyejikusuru hadi akamaliza masomo yake ya chuoni na kuhitimu vizuri akiteseka eti kisa na maana hakuna ajira. Suala la ajira kwa wanaofuzu ni jambo ambalo serikali inafaa ilichangamkie haraka iwezekanavyo. Watu wengi wenye vyeti vyao na maarifa yao wameishia kujihusisha na uhalifu ili tu kulisukuma gurudumu lao la maisha sababu kuu ni kwamba wametamaushwa na serikali kwa kunyimwa ajira." Neema

alisema kwa mfadhaiko. "Ni heri twende kule Uarabuni tukabaguliwe huko kuliko tuendelee kuzama katika bahari ya ***uhawinde.*** Huko tutanyenyekea tu kama nyasi iinamavyo pindi inapokanyagwa" Nami nikasema baada ya kitambo kifupi cha kumpa Neema masikio yangu.

Tangu kuzaliwa kwangu sikuwa nimewahi safiri kwa ndege. Niliona tukio hilo kuwa la kipekee na adimu kabisa maishani mwangu. Angalau katika historia yangu au wasifu wangu ingeandikwa kuwa Yohana aliwahi kwenda Uarabuni kwa ndege. Mandhari hayo mapya niliyobahatika kuyaona siku hiyo yalinishangaza na kunipa pumbao zaidi. Anga lililokuwa tulivu lilituhakikishia safari njema kabisa. Mawingu niliyoyaona kwa ukaribu mno yalikuwa meupe pepepe kama theluji. Kamwe hayakuthubutu kutununia hata kidogo. Yumkini nayo yalikuwa yakiifurahia safari yetu hiyo. Nilisuudika kuona vilele vya milima mirefu mirefu na majengo marefu marefu, zote zikiwa karibu nasi kabisa. Vitu mbali mbali vilivyokuwa ardhini vilionekana vidogo zaidi. Watu kwenye ardhi walionekana kama wadudu wadogo zaidi ambao ili uwaone tu ungehitaji kuwa na ***hadubini***.

Safari hiyo ya ndege iliwapumbaza wengi wakapumbazika. Wengi wakaanza kusinzia huku wengine wakiwa wanalala wakikoroma na kuforota kwa sauti za kutisha. Wengine kama mimi na Neema tulikuwa ***amilifu*** kabisa. Mimi nilijishughulisha na kusoma kitabu chake *Prof. Ken Walibora* kilichoitwa *Siku Njema*. Kitabu nilichokipenda na ambacho nilishinda nikikisoma tena na tena. Uhondo wacho haungenipa nafasi ya kulala wala kusinzia hata kidogo. Akilini nikawa nasafiri na mhusika *Kongowea mswahili* kutoka Tanga kuja hadi Mombasa na hatimaye *Kitale Makutano* kwa *Ngozi*. Mkononi Neema naye alikuwa kashika kitabu chake *Shaaban Robert* kinachoitwa *Kusadikika*. Kayanatisha macho yake kwenye hicho kitabu kama sumaku. Nadhani hakutaka ujumbe uliopitishwa kwenye kitabu hicho ***umfutu*** hata chembe. Sijui ilikuwaje

kwamba sisi sote tulikuwa ***maashiki wa*** kusoma vitabu hususan vya fasihi? Tena vya Kiswahili?

Safari iliendelea bila walakini wala hitilafu yoyote. Nasi tukaendelea kujisomea bila kutatizika kwa lolote wala chochote isipokuwa mikoromo ya waliokuwa katika dunia yao wakila ***usono***. Mikoromo hiyo ilitosha kabisa kumkurupusha simba kwenye himaya yake. Wapo waliozungumza usingizini ila waliokuwa wakizungumza nao ndio sikuwa na uwezo wa kuwatambua. Yumkini ilikuwa mizimu ya Jamaa zao waliokwishatangulia mbele za haki. Wengine walipiga nduru nadhani kutokana na majinamizi waliokutana nayo usingizini.

Baadaye tuliamua kupumzisha akili zetu. Tukaendeleza mazungumzo yetu. Katika mazungumzo hayo tulihadithiana na kusimuliana mengi kuhusu yaliyopita, yaliyokuwepo na tuliyoyatazamia katika siku za halafu. Katika mazungumzo hayo nikamtathmini Neema nikaondokea kumweka katika orodha ya mabinti jasiri, ***adibu*** na wenye bidii maishani. Aidha, nilimuona kuwa aliyejitambua. Hakuwa mwepesi wa kuyumbishwa na vishawishi vya wanaume ovyo ovyo. Sera alizoziandama zilikuwa hirizi zilizomkinga dhidi ya hila na maovu mengi ya dunia. Nikaondokea kumhusudu kwa tabia zake za kuvutia. Alikuwa miongoni mwa mabinti wachache sana wanaojituma maishani. Kamwe hakuwa mwanamke mzembe ambaye ndoto yake ilikuwa kuchumbiwa au kuolewa na mwanamume tajiri. Alitafuta utajiri wake mwenyewe tena kwa hali na vile vile mali.

Kukutana kule na Neema kukawa chanzo cha mkabala baina yetu wawili na urafiki wetu wa kudumu. Hata tulipofika kule Uarabuni baada ya takriban saa kumi za kusafiri, tulimshukuru Mungu kwa safari njema na kisha tukabadilishana namba za simu. "Neema mimi nikutakie kheri sasa. Nakuombea nyota ya jaha. Ukapate kazi, na iwapo baada ya kupata patatokea nafasi nyingine ya kazi naomba ukanifahamishe kupitia nambari

hiyo ya simu. Naahidi kufanya vivyo hivyo pia. Tusisahau udugu wetu wa kiafrika. Udugu wa nikune nikukune tukunane." Nilimsisitizia Neema kisha akajibu, “Ahsante sana Yohana. Kwamba nina namba yako sitakosa kukupigia simu. Nakutakia kheri vile vile ukafanikiwe." "Ahsante sana!" Nikajibu na kisha tukaagana. Kila mmoja akishika njia yake.

Kila nilipopita nilikodolewa macho na kupigwa picha ovyo ovyo na Wazungu na Waarabu- raia wa huko. Nadhani walishangaa kumuona mtu mweusi kama mkaa. Nilipata kusikia baadhi ya minong'ono yao wakisema, "*Look at that monkey! Has it run away from the zoo?"* Walisema na kuulizana huku wakiangua vicheko. Hilo halikunigusa popote madhali tayari nilijua hayo ndiyo ningekabiliana nayo nifikapo kule Uarabuni. Nilikuwa tayari kukabiliana nayo. Niliona bora nijishughulishe na yaliyonihusu.

Mawasiliano baina yangu na mke wangu Fatuma yaliendelea. Nikimfahamisha jinsi safari ilivyokuwa na kuhusu mandhari hayo mageni. Hata punde tu ndege ilipotua katika uwanja wa ndege kule Uarabuni nilitangulia kumfahamisha kupitia simu kwamba nilifika salama salimini. Neema alitangulia kuajiriwa kama mjakazi katika boma la muarabu fulani katika moja kati ya miji mikuu Uarabuni. Hili hakulinyamazia. Alinijuza nami nikamjulisha kwamba nilifaulu kupata kazi ya ubawabu katika boma la mzungu pia kwa usaidizi wa mawakala. Mbali na kudumisha mawasiliano yangu na mke wangu Fatuma, ***sikuyatelekeza*** yangu na Neema. Tulizidi kujuliana hali mara kwa mara. Tukitiana moyo na kutakiana kheri maishani mipango na nia yetu sote ***itengemae,*** kwa kutimizika kwa malengo na maazimio yetu.

# *Sura ya tatu*

Katika boma la *Tom Johnson*-mzungu niliyefanya kazi ya ubawabu kwake, kulikuwa pia na mjakazi mwengine mwafrika. Aliitwa Peter. Yeye katika boma hilo alifanya kazi ya usafi. Uwepo wa Peter katika boma hilo ulinifanya nijihisi nyumbani mbali na nyumbani kwa kukutana na mtu mweusi kama mimi. Angalau tungezungumza mengi yaliyotuhusu sisi waafrika. Aghalabu Peter alipomaliza kazi yake ya usafi alikuja pale getini kukaa na mimi. Pale tungehadithiana mengi ikiwemo chanzo na sababu ya ujio wetu Uarabuni.

Alasiri moja Peter alikuja pale getini. Ilikuwa ndio mwanzo mwanzo wa kufahamiana kwetu. "Uarabuni huku wakuonaje kaka? Peter aliuliza. "Shwari tu kaka ijapokuwa ningali katika kurasa za mwanzo mwanzo wa eneo hili. Bado sijapafahamu vema," nikajibu. "Usijali, utapafahamu tu kaka, lakini naomba nikuondoe hofu. Huku ni kuzuri ijapokuwa ubaguzi wa rangi tu. Sisi watu weusi wanatuona tumbili. Hata hivyo bosi wetu ni mtu mwenye utu wake, kakirimiwa wema chungu nzima. Neno ubaguzi halipo kwenye kamusi yake. Sijui ni kwa sababu amemuoa mwanamke mwafrika au?" Peter alisema. "Amemuoa mwafrika?" nikadakia kwa kuuliza. "Naam amemuo mwafrika tena kutoka nchini kwetu Hawinde. Mke wake anaitwa Huruma. Inasemekana kukutana kwake na bosi, alikuwa kaja huku Uarabuni kusoma baada ya kupata ufadhili. Wakakutana na bosi chuoni na hapo ndipo mchakato wa uhusiano wao kufanyika ndoa ulipong'oa nanga. Bosi na mke wake ni watu wenye utu wema kabisa," Peter akanihakikishia.

"Bosi mwenyewe anafanya kazi gani? Wajua tangu nije hapa nimewahi kumuona nadhani mara moja tu yeye na mkewe!" nikauliza. " Bosi ni mhandisi na mke wake ni wakili. Wao huonekana hapa kwa ***tukizi*** mno kutokana na kazi zao ambazo huwanyima muda wa kutulia hapa

katika boma lao," Peter akanijibu. Matamanio yangu ya kukutana na kuonana ana kwa ana na hao waajiri wangu yalinijia ghafla hasa baada ya kuambiwa kuwa *Tom Johnson* alikuwa mhandisi. Tena mhandisi mwenzangu. Niliamini kuwa angenifaa kwa mafao maridhawa. Ningempa cheti changu akione aamini madhali kuona ni kuamini. Halikadhalika, nilitamani nikamuone mke wake huyo mwafrika ili tupate kujuana na kufahamiana vema. Nadhani angefurahia kukutana na mwafrika mwenzake, tena wa kutoka nchi moja naye.

Kadri siku zilivyozidi kusonga ndivyo tulivyozidi kufahamiana zaidi na Peter. Niligundua kuwa tulitoka katika moja. Nchi ya Hawinde. Kadhalika, vijiji tulivyotoka vilikuwa pua na mdomo. Katika mazungumzo yangu naye, Peter aliukabilisha muda wake kunielezea mengi yaliyomhusu. Alinieleza yote yaliyomhusu; ya raha na karaha kuanzia ukoko hadi utandu. Akanieleza kuwa alifaradhika kuja Uarabuni baada ya maisha kumwia magumu hasa pale alipopatwa na mtamauko mkubwa mno; alipoachwa na mke wake aliyemsomesha hadi chuo kikuu.

Mkewe alipohitimu masomo ya chuo kikuu na kupata ajira ***akamtalaki***. Akamwacha yeye na vikembe vyao viwili. Wana aliozaa na mumewe Peter. Alidai kwamba mumewe Peter hakuwa tena ***kufu*** yake madhali alijiona kuwa mwenye kisomo cha juu kuliko mumewe Peter. Peter alikuwa ameuza shamba ekari moja alilolimiliki ili tu akamsomeshe mkewe akijua kwamba mkewe atakapomaliza masomo yake atamsaidia wakanunue shamba lingine ila maskini hilo halikutimia. Shamba na kila kitu alichokiuza ili akamfanikishie mkewe masomo, vyote vilikuwa vimeenda sasa kwa mganga na havingerudi tena. Waama kiendacho kwa mganga hakirudi. Kuanzia kipindi hicho Peter akaona kwamba maisha hayakuwa maana tena. Yalikuwa sawa na kaka tupu la yai tu. Kila kitamu alichokionja kilikuwa kichungu mithili ya shubiri. Vichungu navyo vilikuwa vichungu zaidi.

Peter alipowazia kujitia kitanzi aliwahurumia wanawe akaghairi nia. Akaamua kumeza mate machungu tu kwa ajili ya wanawe wawili aliowachiwa. Alihisi kwamba endapo angechukua hatua hiyo wanawe wangetaabika sana. Hawangekuwa na mlezi. Mama yao katili alikuwa amewatema kama masuo baada ya kusukutua. Ndipo alipoamua kuwapeleka wanawe kwa nyanya na babu yao- wazazi wake Peter, ili aje Uarabuni kutafuta kazi akawaridhishe wanawe kwa malezi yanayostahili. Mwanamke huyo katili hakuwa na shukrani kwa wema aliotendewa na mumewe Peter hata chembe tu. Kumzawidi mumewe Peter mateke ndilo aliloliona bora. Akashupaza shingo, akayafumba macho yake, masikio akayatia nta na kuuhayawanisha moyo wake. Asione, asisikie wala kuhisi hata chembe chembe za fadhila alizotendewa na Peter.

Nilimuonea Peter imani kubwa kwa mtamauko huo wa kuatua moyo hadi nikadondokwa na machozi. Kamwe hakustahili kutendewa uhayawani huo. Siku zote nikimtia moyo na kumhimiza kuyasahau hayo yaliyopita ambayo hayakuwa ndwele. Nilimhimiza ayagange yajayo madhali hayo yaliyopita yangeendelea kumuumiza na kumnyima amani ya moyoni endapo angeendelea kuyawazia. Nami vile vile nilimuelezea Peter chanzo cha ujio wangu Uarabuni pamoja na maelezo kadhaa yaliyonihusu ambayo yalikuwa sehemu ya utambulisho wangu kwake. Katika maelezo hayo, niligundua kuwa Peter alimfahamu Fatuma barabara baada ya kumwambia kuwa nilimwacha mke wangu anayeitwa Fatuma nyumbani kwetu. Aliniambia kuwa walisoma shule moja ya msingi ijapokuwa yeye alimpiku Fatuma kwa madarasa mawili.

*                    *                    *

Mazungumzo baina yangu na Fatuma mke wangu yaliendelea. Haingepita hata siku moja bila ya sisi kuzungumza. Aghalabu nikimtumia yeye na wazazi hela za matumizi. Wote wakinishukuru mno na kunitakia kheri ya mafanikio. Sahibu yangu wa kike-Neema, naye nilizungumza naye mara kwa mara. Kadri tulivyoendelea kuzungumza ndivyo moyo wake Neema uliondokea kunidondokea kwa mahaba maridhawa. Usemi kwamba hakuna mkate mgumu mbele ya chai ulikuwa tayari ushanipambaukia bayana. Abadani sikutaka nilainike mbele ya chai hiyo-Neema. Iwapo ningelimatia hata kidogo ningeondokea kumkosea Fatuma kwa kuanzisha uhusiano wa kimapenzi na Neema. Niliona bora nimtaarifu Neema mapema kwamba nilikuwa tayari na mke ili isijetokea madhara mabaya ya chelewachelewa.

Neema alikuwa mwepesi wa kuelewa na wala hangeruhusu taarifa yangu hiyo iuvunje urafiki wetu huo mkubwa. Tuliendelea kuwa marafiki wa chanda na pete. Tukafaana kwa vingi na katika nyakati zote. Si za mvua, si za jua, si za mwanga, si za giza. Ndio uliokuwa urafiki wetu siku zote.

Baada ya siku tatu Neema alinipigia simu akiwa na bashasha mno. Alinijulisha kwamba alikuwa amepata kazi aliyoisomea; kazi ya uhasibu. Alinieleza kwamba muajiri wake ndiye aliyemtafutia kazi hiyo baada ya kugundua kuwa alikuwa na shahada ya uhasibu. Katika mawasiliano hayo nikampongeza Neema kwa ufanisi huo. Vilevile nikamtakia heri katika kazi hiyo. Halikadhalika, naye hakusita kunitakia kheri. Akanipa moyo kwamba nami siku yangu itafika. Neema aliitumia nafasi hiyo barabara. ***Alilimbika*** hela alizozipata katika benki ili zikamfae kwa maendeleo yake ikiwemo kuwasaidia ndugu zake na kuwainua babu na nyanya yake. Mshumaa wa matumaini ya nami ***kusuudika*** kupata ajira katika kozi niliyoisomea chuoni haukuzima. Ulizidi kumwaya mwanga. Siku zote mwanga huo ukinifariji na kuniondolea hofu moyoni hata nilipoelekea kukata tamaa.

# *Sura ya nne*

Moja kati ya siku za mapumziko nilifunga safari na Peter kwenda kutembea katika mji mmoja maarufu kule Uarabuni. Ulikuwa mji wenye haiba ya kipekee. Majengo marefu marefu na usafi wa mji huo ulinivutia mno. Kilichonichukiza na ***kuuvuaza*** mtima wangu ni kile kitendo cha ubaguzi dhidi ya mwafrika kilichoshamiri katika mji huo. Mtu mweusi hakufaa kabisa mbele ya macho ya mtu mzungu. Alikuwa kama kopo la msalani au pengine kiumbe cha ajabu zaidi na ndio maana wazungu hao walishinda wakitukodolea macho kwa mshangao mkubwa. Walikuwa kama waliosuudika kuyaona mabaki ya Adamu na Hawa.

Ukweli kwamba rangi ya mtu na asili yake ni pambo tu la kimaumbile na hazipaswi kuwa sababu ya kubaguana kamwe haukuwaamshia wale wazungu wenye mioyo miyeusi kama mkaa hisia zozote za utu. Niliitikadi kwamba inawezekana utu umewakimbia watu na kuwaingia wanyama nao unyama ukawakimbia wanyama na kuwaingia watu. Si maajabu kumuona mbwa akimkuna ng'ombe kwa upendo wa dhati tena bila kumjeruhi kwa njia yoyote ile. Vile vile si maajabu kumuona binadamu akimuangamiza binadamu mwenzake kwa silaha hatari bila kujali wala kubali. Matendo ya kiuhayawani ulimwenguni yamekuwa kawaida tu. Kefule! Maajabu kweli!

Kila tulipopita Wazungu na Waarabu ambao walikuwa raia wa huko walituepuka kama kwamba tulikuwa na ugonjwa wa Ukoma. Hawakukubali tuwakaribie. Walishinda wakizipepea pua zao kwa viganja madhali walituona kama tulionuka harufu mbaya ya kutisha. Wengine walikuja mbele yetu kutupiga picha huku wakichekacheka kama kwamba walikuwa wakiwafurahia sokwe katika mbuga ya wanyamapori. Watoto wao wadogo walitukimbia huku wakilialia kila walipotuona. Hatukuruhusiwa kupita karibu na maduka madhali walituona wezi.

Nilivuta taswira ya kwetu Afrika na jinsi sisi waafrika huwapokea wazungu kila wajapo katika bara letu nikaona kwamba sisi waafrika tumestaarabika kwa kiwango kikubwa zaidi tukilinganishwa na wazungu. Wazungu wajapo katika bara letu la Afrika sisi huwaona kama wageni na watalii wanaostahili staha lakini Waafrika katika bara lao huchukuliwa kama wakimbizi. La kushangaza zaidi ni kwamba hata wazungu hawa huabudiwa kama miungu na baadhi ya Waafrika wajapo katika bara letu. Maskini sisi! Abadani hatukuwa kama wazungu wanaotudhalilisha sisi waafrika tuzurupo bara lao. Badala ya kutupokea kwa njia nzuri wao siku zote ***wanatunyanyapaa.*** Katika mojawapo ya maduka ya nguo yaliyokuwa katika mji huo, niliona gauni iliyonivutia mno. Niliona kwamba ingemfaa zaidi mwendani wangu Fatuma. Nilimuomba Peter tusonge karibu na duka hilo ili niweze kuliona vazi hilo vizuri na niulizie pia bei yake.

Mlangoni mwa duka hilo tulimkuta bwana mmoja mwenye asili ya kiafrika aliyekula akashiba. Kiriba kilichojitokeza bayana na mashavu yake yaliyojaa yalidhihirisha hilo. Rangi ya ngozi yake ilikuwa ya hudhurungi. Kwa muonekano wake alikuwa mwafrika halisi kabisa. Alikuwa kavalia, viatu vizito vyeusi, suruali ndefu nyeusi, chepeo nyeusi na shati nyeusi iliyokuwa na nembo iliyoandikwa *security.* Nembo hiyo na kifaa cha kukagulia watu wanaoingia dukani kubaini iwapo wana silaha hatari ilitosha kutuhakikishia kwamba alikuwa ndiye mlinzi katika duka hilo. Tulikaribia katika mlango wa duka hilo bila hofu yoyote madhali tuliamini kwamba mwafrika mwenzetu hangetudhulumu kwa ubaguzi wa rangi wala asili. Tuliamini angetupokea na kutukaribisha vizuri katika duka hilo.

"Habari yako ndugu?" nikamuamkua kwa bashasha na kisha kusubiri jibu la salamu. Baada ya muda mrefu wa bwana yule kunitumbulia macho kwa ghadhabu bila kujibu salamu yangu niliamua tena kumuamkua kwa

mara ya pili sasa. Makisio yangu yakiniambia kwamba pengine hakuwa amenisikia. Sikutaka kutumia lugha ya kingereza madhali niliamini kuwa alikuwa anaifahamu lugha ya Kiswahili, "Hujam..." Hata kabla ya kumalizia salamu akanikatiza kwa ghadhabu, "*You monkey! What do you want here? I think you are thugs. Let me call the police right now.*" Tulijitahidi kujitetea kwake, "*No brother. We do not have any evil intenstion. We just came here to inquire the cost of this dress," nilisema* huku nikiashiria gauni hiyo kwa kidole changu kilichokuwa kikitetemeka kwa lililotupata. Peter naye alipojaribu kutetea nia yetu mahala hapo, akazabwa kibao shavuni.

Nilimuangalia mlinzi huyo kwa hasira za simba aliyejeruhiwa. Nikazidhibiti hisia hizo za hasira ili zisinifanye nivaane na bwana yule vibaya vibaya. Nilimhurumia na kumsikitikia Peter zaidi. Hata baada ya kuzabwa kibao hicho Peter hakuthubutu kurudisha baya kwa baya. Alimeza mate machungu tu na kisha kutulia. Kujitetea kwetu kwamba hatukuwa na nia yoyote mbaya mahala hapo kulikuwa tasa. Hakukutuzalia matunda kabisa na hivyo basi hatukuwa na budi kusubiria hatima yetu mbovu.

Hata bila ya huruma kwetu mlinzi huyo alibofyabofya simu yake upesi na kuwapigia askari simu. Baada ya muda mfupi ***karandinga*** lilikuwa limekwishafika mahala hapo, tayari kutuchukua. Hapo tukafungwa pingu na kusukumwa mbio mbio hadi katika karandinga hiyo. Tulipofikishwa katika kituo cha polisi tulifungiwa katika chumba kimoja kilichokuwa na chungu walionona na kunoneana. Ilisemekana wadudu hao waliwekwa mle ndani mahususi kututia adabu. Sijui sasa adabu gani? Chumba chenyewe kilikuwa na baridi ya mzizimo. Halikadhalika mwanganza mle ndani uliadimika kama wali wa daku. Kiza cha kaburi ndicho kilichotawala mle ndani. Humo nikafungiwa na Peter tukabiliane na baridi hiyo kali pamoja na adhabu kali ya chungu hao hatari.

Wahalifu wazungu walifungiwa katika chumba kizuri kilichokuwa na kitanda pamoja na runinga. Hakikuwa na baridi wala chungu kama chetu Waafrika, maskini ambao hatukuwa na hatia yoyote. Siku iliyofuata tukapelekwa kortini ambako tulihukumiwa kwa tuhuma ya wizi wa kimabavu. Kosa ambalo hatukuwa tumeliwazia wala kulitenda. Hatukuwa na jinsi ila kuridhia dhuluma hizo dhidi yetu Waafrika. Kortini hakimu mzungu akatuhukumu kifungo cha miaka mitatu kwa masingizio tu.

Niliondokea kumchukia mlinzi huyo kadri ya uwezo wa moyo wangu hadi hii leo. Nilikerwa kwa jinsi alivyoutukanisha uafrika wake kwa kutusababishia karaha ile. Sikutaraji kuwa angetutendea udhalimu huo bila kuzingatia kwamba tulikuwa waafrika wenzake au binadamu wenzake basi. Kuanzia hapo nikaondokea kumuafadhalisha mbaguzi mzungu kuliko mbaguzi mwafrika. Nafsini nikijiuliza ujamaa na undugu wa waafrika ulitokomea wapi? Yumkini ukoloni ulitupagawisha na kutufanya tusahau uafrika wetu ulioshamiri utu, undugu na mshikamano. Inasikitisha kwamba waafrika wengi wamekuwa wazungu bandia mathalani mlinzi huyo wa duka la nguo. Wanaizungumza lugha ya Kiswahili iwe yawe tu! Wengine hawaizungumzi kabisa. Wanahisi kwamba utakuwa ushamba kuizungumza lugha ya Kiswahili. Inasikitisha na kutamausha kweli kwamba baadhi ya waafrika wameondokea kuwa watumwa hadi wa lugha.

* * *

Huruma-mke wa bosi wetu alipopata taarifa kwamba tulikuwa tumeshikwa na kuhukumiwa alikuja kutuokoa. Ushawishi wake mkubwa katika masuala ya sheria mjini humo ulitufaa zaidi. Alitutetea tukaachiliwa huru kwa dhamana. Akatusikitikia na kutuonea huruma zaidi kwa kuhukumiwa kwa masingizio baada ya yeye kugundua baadaye kuwa hatukuwa na hatia yoyote. Alipotaka kumshitaki mlinzi huyo tukamrai amsamehe. Hatimaye tulirudi katika boma lake kuendelea na kazi.

# Sura ya tano

"Poleni sana kwa yaliyowakuta vijana wangu," bi Huruma alisema kwa lafudhi iliyoathiriwa zaidi na lugha ya Kingereza. "Ahsante. Tushapoa," nikajibu na Peter kwa pamoja. Bi Huruma alikuwa ametuita katika kikao ukumbini mwa jumba lake la kifahari. Tangu nianze kazi katika boma lake hilo sikuwa nimewahi kaa naye kwa mazungumzo kutokana na ratiba yake iliyomnyima muda wa kukutana na kuzungumza na mimi. Ukumbi wa jumba lake hilo la kifahari ulipambwa ukapambika. Kwenye kuta kulitundikwa picha zenye haiba ya kipekee zikiwemo picha zake, wanawe na mume wake Tom Johnson. Vyombo vya samani vilivyotengenezwa kwa ufundi na ujuzi wa kiwango cha juu ikiwemo meza na makochi vyote vilinivutia si haba. Vyote hivyo vilikuwa vya bei ghali. Halikadhalika nilipendezwa na runinga kubwa ajabu mithili ya ubao wa kufundishia wanafunzi shuleni iliyotundikwa ukutani.

"Kwamba ulifika na kuanza kazi uliyoelekezwa kuifanya katika boma langu hili ni jambo ambalo nalifurahia mno. *Personally, I was very busy in the court when you came.* Nilimtuma *agent* akanitafutie mtu atakayefanya kazi ya ubawabu katika boma langu hili *and am very greatful that he found you."* Bi Huruma aliniambia kwa Kiswahili na Kimombo. Ilimwia vigumu kuzungumza kwa lugha ya Kiswahili bila kuhusisha lugha ya Kingereza kutokana na kuishi uzunguni kwa miongo mitatu. Jambo ambalo lilimfanya aathirike zaidi na lugha ya Kingereza.

"Mimi naitwa Huruma mkewe Tom Johnson. Mimi ni mwafrika kama nyinyi. Nilitoka nchini Hawinde takriban miaka thelathini na tatu iliyopita kuja kusomea huku masomo yangu ya chuo baada ya kupata ufadhili wa kusomea sheria. Nilikuwa miongoni mwa wanafunzi bora katika mtihani wa kitaifa na ndio maana serikali ikanipa mimi na wengine ufadhili wa kusomea huku. Mume wangu Tom Jonson nilikutana naye katika chuo

ambako tulikuwa twasoma pamoja. Yeye alikuwa anasomea uhandisi wa ujenzi wa miundo msingi. Tuliondokea kuchumbiana hadi tukaoana baada ya kuhitimu masomo yetu," Bi Huruma alijitambulisha zaidi na kisha akaniomba nami nijitambulishe.

Kabla ya kuanza kujitambulisha, niliisafisha koo yangu kwanza madhali kama nilivyomuona Bi. Huruma alitarajia maelezo mengi ya utambulisho toka kwangu.

"Mimi ninaitwa Yohana. Asili yangu ni bara la Afrika katika nchi iitwayo Hawinde..." Bi Huruma aliposikia kwamba nilitoka katika nchi ya Hawinde akanikatiza na kuniuliza ili ahakikishe, "Eti *you are from* Hawinde?" "*Yes, I am from* Hawinde," nikajibu kisha Bi Huruma akaunyosha mkono wake kwa furaha na kunisalimu ishara ya kufurahia kwamba mimi na yeye tulitoka nchi moja. Baadaye niliendelea kijitambulisha, "Nimekwishahitimu masomo yangu ya chuo kikuu baada ya kutaalumia uhandisi wa ujenzi wa miundo msingi. Nina mke ambaye nilimwacha nyumbani kwa wazazi wangu ambaye naye amehitimu baada ya kutaalumia uhasibu. Uhaba wa ajira nchini ndio umenishurutisha kuja huku kutafuta kazi," nilimalizia utambulisho wangu.

Bi Huruma aliposikia kwamba nilikuwa nimetaalumia uhandisi, aliahidi kunitafutia kazi. Stakabadhi na vyeti vyangu vyote nilikuwa nimevibeba katika mkoba wangu madhali niliona kwamba vingenifaa baadaye kule Uarabuni. Licha ya Bi Huruma kukaa Uarabuni kwa muda mrefu hivyo bado aliutanguliza na kuukumbatia undugu wa kiafrika. Hakuwa ameruhusu utamaduni na mtindo wa maisha ya kule Uarabuni zimshupaze shingo wala zimsahaulishe udugu huo wa kiafrika. Hakuwa kama 'wazungu bandia' walojitwika na kujipakaza uzungu usio wao, hata wakawaona waafrika wenzao kama tumbili. Wakaondokea kuwaamshia ***zani*** pamoja na kuwasababishia karaha bila hatia wala kosa lolote. Watu

kama bi Huruma wameadimika sana katika dunia ya leo. Katika elfu waweza pata mmoja tu au hata umkose kabisa. Waja wengi wamehayawanika wakasahau utu kabisa.

"Wajua mataifa mengi yanayoendelea hususan barani Afrika hayajachangamkia sana upanuzi au uzalishaji wa nafasi za kazi kwa watu wao. Halikadhalika, ubinafsi wa viongozi na mapendeleo katika kuajiri watu zimechangia kwa asilimia kubwa kuwepo kwa tatizo hili la uhaba wa ajira kwa watu wengine wenye vyeti na maarifa. Hii ndio sababu ya watu wengi kutopata kazi hata baada ya kukamilisha masomo yao chuoni na kutimiza vigezo vyote vya kuajiriwa. Baadhi ya viongozi huajiri watu wa familia yao au wa kabila lao ambao hata hawajatimiza vigezo vya kuajiriwa- hawana elimu na maarifa inayohitajika katika kufanya kazi hizo huku walioafiki vigezo hivyo wakiachwa nje." Bi Huruma alisema. "Ni kweli kabisa mama," nikaridhia bila pingamizi yoyote kwa aliyoyasema. Ulikuwa ukweli mtupu.

Bi Huruma aliendelea,"Kwamba nimeamua kukusaidia ukapate kazi ya uhandisi kuku huku Uarabuni hufai kutia shaka. Nitahakikisha kwamba umeipata kazi hiyo." "Nitashukuru zaidi mama," nikasema. Ahadi hiyo ilinipa nguvu zaidi. Angalau nikaiona kesho yangu ikiwa na mwanga uliozagaa katika kila kipembe cha maisha yangu ya halafu. Angalau ningekuwa na kazi yenye hadhi tena yenye mshahara mkubwa zaidi. Nilikula yamini kuuvumilia ubaguzi wa rangi uliokithiri Uarabuni hadi ndoto zangu zikatimie. Ningewanyamazia wale wangenisema vibaya vibaya au hata kunitukana eti kisa na maana mimi ni mtu mwafrika; mtu mweusi.

Jioni moja Tom Johnson alipofika hapo nyumbani kwake toka kazini, mkewe bi Huruma alikuwa na tonge la kummegea. Lipi lakini? Naam, wasifu wangu! Alimueleza kuhusu usuli wangu, kisomo changu kilichohusisha taaluma niliyoisomea chuoni pamoja na chanzo cha ujio

wangu Uarabuni. Mumewe aliposikia kwamba nilikuwa na shahada ya uhandisi wa miundo msingi sawa na yeye akanifurahia sana. Akanisikitia alipogundua kwamba licha ya kuwa msomi niliishia kukosa kazi katika taifa langu na kuishia Uarabuni kufanya kazi iliyoitukanisha kabisa kisomo changu hicho; kazi ya ubawabu katika boma lake. Bosi alihisi kwamba haikuhalisi kabisa mimi na shahada yangu ya uhandisi kufanya kazi kama hiyo. Aliona kwamba huko kulikuwa sawa na ***kuitehemu*** elimu inayotupa maarifa na kutupa kazi zenye hadhi. Mwenyewe alipenda elimu mno na asingependa kuona elimu ikivunjiwa heshima yake.

Jioni hiyo alimtuma mkewe bi Huruma aje aniite. Wakati huo nilikuwa nimetulia tu pale getini nikiyawazia maisha yangu ya nyuma, ya wakati huo na ya usoni. Nyuni walishinda wakirukaruka toka mti mmoja hadi mwingine huku wakilialia kwenye miti iliyoizunguka boma hilo. Katika mawazo hayo mazito, nikashtuliwa na kinyesi cha nyuni mmoja aliyeniendea choo utosini. Nikagutuka na nilipoinua kichwa changu nikamuona Bi.Huruma roshani akiniita kwa ishara akitumia mkono wake wa kulia. Nikanyanyuka upesi na kwenda alikokuwa haraka huku nikiwa na mseto wa mawazo.

Nilikuwa nikiwazia alichoniitia pamoja na tukio hilo la nyuni. Katika jamii yetu nchini kwetu Hawinde, ilikisiwa kwamba nyuni akikuendea choo kwenye kichwa huwa ni ishara ya bahati njema. Wengi waliamini hivyo na ama kweli waliondokea kubahatika kila walipoendewa choo na nyuni. Hata hivyo imani ina nguvu ya kufanya visivyowezekana viwezekane. Katika Bibilia Petro alishindwa kutembea juu ya maji kutokana na imani haba. Iwapo angekuwa na imani kama ya Yesu inawezekana angefanikisha jaribio hilo. Basi nikatamani makisio na imani ya jamii yetu ikatimie kwangu kutokana na tukio hilo la nyuni.

Nilipanda upesi vidato vya jumba hilo la kifahari hadi kwenye roshani, alipokuwa bi Huruma. Pale akanisalimu na kuniagiza nimfuate. Akanielekeza hadi katika chumba kimoja alimokuwa mumewe. Kwa muonekano wacho kilikuwa chumba cha kusomea. Tuseme maktaba ndogo ya nyumbani. Mle mlikuwa na vitabu nui mbali mbali vilivyopangwa katika vijisanduku vidogo vidogo kwenye ukuta; si vya kiada, si vya hadithi, si kamusi ya Kiswahili na Kingereza. Kilichonishangaza na kunivutia zaidi kwa wakati mmoja ni milki kubwa ya vitabu vya Kiswahili hasa vya hadithi alivyokuwa navyo. Mle chumbani Tom Johnson alikuwa akisoma kamusi ya Kiswahili. Tukio ambalo lilinishangaza na kunitafakarisha zaidi. Nilishangaa jinsi mzungu alivyojitutumua kuifahamu lugha ya Kiswahili huku wazungumzaji asilia wa Kiswahili ***wakijitutumua*** siku zote ***kuitehemu*** lugha ya Kiswahili badala ya kuiboresha na kuiendeleza. Hata hivyo moyoni nilifurahi na kufarajika mno kwa jinsi Kiswahili kilitambulika hadi Uarabuni na Ughaibuni.

Kwa jinsi nilivyomuangalia mumewe bi Huruma kwa mshangao mkubwa, ilimwia rahisi kutambua kwamba nilikuwa nimeshangazwa naye kwa tukio hilo la yeye kusoma kamusi ya Kiswahili. Tukio nililoliona la ajabu sana. Aliniangalia kwa tabasamu kisha akaisafisha koo yake na kusema kwa Kiswahili chenye lafudhi iliyoathirika mno na lugha ya Kingereza, " Karibu uketi mwanangu," "Ahsante mno!" nikashukuru na kuketi kwenye kochi lililokuwa mkabala na alilokalia yeye na mke wake bi Huruma. Kisha akaendelea, "*I know you are surprised seeing me reading Kamusi. Is it?" "Yes sir. Am very suprised,"* nikajibu huku nikitabasamu. "*I like Kiswahili too.* Ninajitahidi niijue Kiswahili. Niongee kwa ufasaha kama nyinyi wenyeji wa *this language. My honey* amenifanya nipende Kiswahili. Ndiye *my teacher," bosi* akasema huku akimgusagusa mkewe bi Huruma begani. Kipindi hicho chote Bi.Huruma alishinda akitabasamu huku akizigusagusa ndevu za mumewe zilizokuwa ndefu.

Maongezi baina yetu watatu yaliendelea katika chumba hicho. Tom Johnson akaniambia kile alichoniitia jioni hiyo mle chumbani. Alisema kwamba alikuwa amesikia maelezo kunihusu toka kwa mkewe na alikuwa radhi kunisaidia kwa hali na mali nipate kazi. Nilienda nikachukua vyeti vyangu vya masomo katika chumba nilichokuwa nikilala aliponiuliza ikiwa nilikuja navyo Uarabuni, nikampa avipitie. Baada ya kuviona na kuvipitia alinipa mkono wa tahania. Akaona kwamba vyeti vyangu hivyo viliakisi na kusadifu upevu wangu wa akili. Akanihongera zaidi. Baadaye aliomba asalie navyo ili siku ambayo ingefuata aende akaniombee kazi katika shirika la uhandisi alilokuwa akifanya kazi nalo. Katika kampuni hiyo, yeye alihudumu kama makamu mkurugenzi.

# ***Sura ya sita***

*Wangu muhibu ninao uhaba,*

*Uhaba wa lako tamu huba,*

*Mno ninalipeza hilo huba,*

*Lini 'tapata hayo mahaba,*

*Unondowe jakamoyo kwa yako mahaba,*

*Uulainishe mtima wangu mahabuba.*

Niliulainisha moyo wake Fatuma kwa wimbo huu kila tulipozungumza. Hata alipokuwa kapungukiwa na furaha au hana furaha kabisa kutokana na ***makuruhu*** ambayo ni faradhi maishani, wimbo huu ulimpa furaha na utulivu wa mtima. Mapenzi ya dhati niliyokuwa nayo kwake yalinifanya niondokee kuwa mraibu wa kuzungumza naye mara kwa mara. Nilijitahidi kuwasiliana naye kwa simu kila nilipoamka na hata kabla ya kulala. Tukijuliana hali na kujulishana kila hatua. Aidha, tulitiana moyo na kutakiana kheri ya siha na mafanikio kila wakati. Mambo yote yaliyokuwa yakiendelea nchini kwetu na nyumbani alikuwa akinifahamisha nami nikimfahamisha ya Uarabuni kupitia mawasiliano hayo. Katika suala zima la ufahamishaji nilimkuna akanikuna na tukakunana. Katu ***halingenifutu*** jambo lolote au tukio lolote kiamboni kwetu na nchini kwetu kwa jumla.

Halikadhalika,tulihusishana katika namna ya kujiendeleza kimaisha katika mazungumzo yetu hayo ya mara kwa mara. Aghalabu nikimueleza mapendekezo yangu yaliyohusu sehemu mwafaka ya kununua shamba ambako tungeishi na aina ya nyumba ambayo tungejenga. Fatuma naye angetoa mapendekezo yake. Alikuwa mbishi mno kwa jinsi nilivyomfahamu. Hangeridhia jambo kirahisirahisi tu. Tabia na hulka yake hiyo Fatuma ilitufanya tuzamie katika majibizano ambayo yangetuchukua

saa nyingi kufikia makubaliano. Wakati mwingine mapendekezo yetu wawili yakikinzana lakini baadaye tungeafikiana kwa hili au lile. Angalau mkinzano wa mapendekezo yetu hayo yangefikia ukomo wake.

Katika mojawapo ya mawasiliano yetu, Fatuma alinijulisha kwamba kulikuwa na nafasi ya kazi ya uhasibu iliyopatikana akaamua kujaribu aone ikiwa bahati ingemwangukia. Fatuma akaomba nafasi hiyo ya kazi kupitia waraka aliouambatanisha na vyeti vyake vya masomo pamwe na stakabadhi zingine muhimu zilizohitajika. Baada ya majuma mawili Fatuma akaitwa katika sehemu hiyo husika kwa usaili. Alikuwa miongoni mwa vijana sita waliochaguliwa kwa usaili baada ya kutuma barua zao za kuomba kazi hiyo. Katika usaili huo Fatuma alikutana na mtamauko uliomuachamisha na kumvunja moyo kabisa. Usaili huo uligeuka uumbuliwaji, dharau na madhalilisho ya nui mbalimbali yaliyoelekezwa kwake. Huko alikutana na jopo la usaili lililokuwa tayari limelishwa mlungura na mmoja wa waliofaa kusailiwa. Ilisemekana kuwa yule aliyelilisha hongo jopo hilo alitoka katika familia ya walala hai na wazee wake ndio waliompa hela za kuwaonga wanajopo hao ili wampe kazi hiyo. Hivyo usaili huo haukuwa na maana yoyote wala manufaa yoyote kwa Fatuma. Ulikuwa kama kaka la yai tu. Laiti angejua mapema ili asijisumbue kuomba kazi hiyo. Ilikuwa sawa na kutaraji jiwe likujibu swali fulani baada ya kuliuliza.

Katika nchi ya Hawinde ulaji wa milungura ulikithiri. Aidha, ulikuwa kawaida kama ibada. Ikiwa ulitaka kupata kazi yoyote ile hata ya kijungu jiko ilikuwa lazima uwe na mkono wa kurambwa. Mahawinde kama Fatuma hawakuwa na lao ila Mungu tu. Lakini inawezekanaje mtu awe na Mungu na akose kufanikiwa katika jambo fulani? Si Mungu hashindwi na lolote wala chochote? Au... Oooh! Yumkini itakuwa ni muda wa Mungu kumtimizia mja huyo yale ayatakayo ndio utakuwa haujawadia.

Naam, muda! Si muda ni dawa mujarabu wa vitushi vya maisha? Basi daima tuuwachie muda kazi yake, utudhihirishie mbivu na mbichi.

Fatuma aliniambia kupitia mazungumzo yetu kuwa katika usaili huo aliishia kuulizwa maswali ambayo hata hayakufungamana wala kuhusiana kabisa na kazi hiyo aliyoiomba. Wakimuuliza kabila lake, kama yuko katika ndoa au bado hajaolewa pamoja na kumuuliza alikuwa mfuasi wa chama gani ya kisiasa; kati ya vyama viwili vilivyokuwa vya mafahali wawili waliokuwa wanagombea kiti cha urais nchini. Halikadhalika walionekana kuwa wenye dharau mno. Walimdharau Fatuma kwa kuwa hakuwa na lake. Viti walivyovikalia viliwatakaburisha. Wakawaona wengine kama ***masimbi*** tu. Nilimsikitikia na kumuonea Fatuma imani zaidi kwa ***maumbufu*** hayo dhidi yake. Hisia hizo za imani nilizokuwa nazo kwake zikanitanabaishia beti mbili za shairi nililowahi kulisoma mahali. Kimyakimya nilijikaririia;

***'Sinione masikini, madharau 'kazidisha,***

***Ukanishusha thamani, na kunifanya dubwasha,***

***Chanzo una vya thamani, bei vinakupandisha,***

***Usinidharau ndugu, kwa kuniona sifai.***

***Yule alekupa kiti, ndiye 'linipa kumbi,***

***Ukiwa katika kiti, usinione masimbi,***

***Kesho nami nitaketi, na yatakwisha mawimbi,***

***Usinidharau ndugu, kwa kuniona sifai.***

# *Sura Ya Saba*

Ushawishi mkubwa aliokuwa nao bwana Tom Jonson katika kampuni hiyo ya uhandisi ulinipa hakikisho la kupata ajira. Siku zote nikiitikadi kuwa katika kufanikiwa matarajio ya kufaulu yanafaa yawe makubwa zaidi kuliko matarajio ya kufeli. Baada ya kupita siku chache hivi, niliajiriwa katika kampuni hiyo ya uhandisi kama Msanifu Ujenzi; taaluma mojawapo miongoni mwa taaluma za uhandisi niliyoisomea chuoni. Kazi hiyo ilihusu uchoraji wa ramani ya majengo mbali mbali. Kazi niliyoipenda na kuionea fahari zaidi. Kwangu kazi hiyo ilikuwa mzigo wa pamba madhali Mungu alikuwa kanitunuku kipaji cha uchoraji. Kauli kwamba Mungu hamtupi wala ***hamtelekezi*** mja wake ikanipambaukia bayana. Nilihisi kuwa *'green pasture'* niliyokuwa nikiimezea mate kwa muda mrefu ilikuwa sasa imetimia. Awali ilikuwa miongoni mwa ndoto zangu nilizoziwazia na kuziota katika ulimwengu wa kifantasia tu. Alhamdulilahi! Sasa ilikuwa katika ulimwengu halisi. Tena halisi kabisa.

Nilianza kuona sasa matunda ya elimu pamoja na tija ya mahangaiko ya muda mrefu shuleni na vyuoni. Nikaona jinsi elimu haina mipaka, kwamba haitambui tabaka, kabila wala uraia. Ni watu tu ndio wenye mipaka na ubaguzi usiomithilika. Watakuambia kuwa elimu na matunda yake ni ya watu walioafiki vigezo fulani fulani tu. Ukiwaambia wakutajie vigezo hivyo utaishia kuwa mja aliyeona jiwe likizungumza. Utapigwa na butwaa kuona jinsi kuna tofauti kubwa kati ya mtu aliyeelimika na aliyeishia kusoma tu. Wengi walioishia kusoma tu ndio waongozao kufanya mambo mengi ya ovyo katika jamii. Hawana michango yoyote ya kupigiwa mifano katika jamii. Walioelimika nao huwa katika mstari wa mbele kufanya mengi ya kuigwa na wengi katika jamii. Wengi wao wana michango hasi tu katika jamii. Huyatumia maarifa waliyoyapata shuleni baada ya kusoma na kuelimika kuleta maendeleo makubwa katika jamii.

Hata wafapo majina yao na michango yao huwa zimeandikwa kwenye uso wa dunia. Hudumu milele na vizazi vya leo, kesho, kesho kutwa, mtondo, mtondogoo na hata milele huwatambua. Aidha, hutambulika katika kila kipembe cha dunia.

Kupitia elimu, mtu yeyote kutoka mahali popote anaweza kuajiriwa mahali popote muradi ana vyeti vya kuthibitisha kwamba ametaalumia kozi fulani inayohusiana na kazi husika. Watu wanapokumbatia elimu huondokana na utumwa wa ujinga kwa kupata mwanga na kuona jinsi dunia ilivyokirimiwa mengi mazuri ambayo bila maarifa ambayo ni matunda ya elimu waja hatuwezi kuyaona. Dunia imejaa fursa. Ukiondoa manyingu na matongo kwa kuelimika utaziona. Elimu ni taa na gizani humwaya mwanga watu wakatazama na kuona vizuri jinsi dunia ilivyo na mengi yaliyo matamu hata kuliko uki. Aidha, mashahidi wa manufaa ya elimu watakwambia, *'Education is the key to success'* - elimu ni ufunguo wa mafanikio.

Nilimshukuru bwana Tom Jonson kwa utele wa shukrani. Bwana yule na mkewe walitunukiwa ***nyoyo kubwa*** ajabu. Wawili hao sikuhusiana nao kwa damu wala usaha lakini kwa jinsi walivyonitendea wema singethubutu kuwasahau hadi mauko yangu. Siku zote nikiwaona kuwa walioumbwa kunitimizia ndoto zangu nzuri. Habari za kuwalipa mashuzi au mateke kwa fadhila walizonitendea kamwe singethubutu kuipa nafasi ya kutokea. Si jema hulipwa kwa jema? Hata mabaya hatupaswi kuyalipa kwa mabaya bali mema.

Kazini nilikutana na watu kutoka mataifa mengine barani Afrika ambao nilifanya nao kazi. Wote wakifurahia mandhari hayo ya Uarabuni hali. Aghalabu, tulizamia katika mazungumzo mazito yaliyohusu ulinganishi wa mataifa ya bara la Afrika na kule Uarabuni. Tuliangazia mawanda mengi ikiwemo; uongozi, thamani ya fedha, umiliki wa rasilimali

mbalimbali mathalani dhahabu, almasi, mafuta, mito,maziwa na hata wanyama pori.

"Hivi mwajua kwamba Afrika ni bara tajiri zaidi?" Akasema Thomas; raia wa nchi ya Watumwa. "Naam, bara la Afrika limekirimiwa vingi sana. Bara letu ni bara tajiri kupita kiasi ila tatizo ni viongozi wetu wasiolinda rasilimali zetu kwa manufaa ya mataifa yetu. Wao watashawishiwa na mataifa ya ughaibuni na kuziuza malighafi na rasilimali zetu kwa bei za kutupa na kisha baadaye kununua bidhaa zilizoundwa kwa malighafi na rasilimali zetu hizo kwa bei ghali mno toka katika mataifa haya haya ya Ughaibuni na Uarabuni. Cha kutamausha zaidi ni kwamba tunauziwa bidhaa zenye thamani ya chini na hafifu kwa bei ghali huku wenyewe wakijiundia zilizo bora na dhabiti kwa rasilimali zetu hizo hizo tu," nikasema na kisha kuendelea huku Thomas na wengine wakiwa wananisikiliza kwa makini zaidi.

"Tunayapiku mataifa ya Ughaibuni kwa vingi mno. Si madini, si maziwa na mito, si wanyamapori, si rasilimali mbali mbali, si... Itoshe tu kwamba bara letu ni tajiri zaidi na tunapaswa kufumbua macho vinginevyo tutaendelea kuwa maskini wa kutupwa huku mataifa ya Uarabuni na Ughaibuni yakiendelea kujitajirisha kwa utajiri wetu. Naamini barani Afrika patazaliwa *Muamar Gadaffi na Magufuli* wengine watakaoionea bara la Afrika fahari na watakaoipigania bara letu hili kwa udi na uvumba kupitia uongozi wao wa kupigiwa mfano. Aidha, ***watakaojitutumua*** kuwakomesha wazungu dhidi ya kuendelea kuifukarisha Afrika kama walivyofanya mashujaa hawa na wengine wengi. Pamoja na fadhila zote ambazo tumeyatendea mataifa haya ya Ughaibuni ni shukrani zipi wametupa zaidi ya ***mashuzi***? Mara kwa mara wanawashawishi viongozi wetu kwa vijisenti kwamba waridhie kuhalalisha ndoa ya jinsia moja. Ajabu kweli! Huu ni ushetani ambao tunafaa kuupinga na kuutokomeza kwa hali na mali."

Aghalabu tulizamia mazungumzo kwa kina tukilitazama bara letu la Afrika kwa jicho la tatu. Kila mmoja wetu alikuwa na hili au lile la kusema kuihusu bara letu. Sarafina mmoja wa wahandisi wenzangu naye alikuwa na lake la kusema, "Thamani ya fedha za Ughaibuni iko juu ikilinganishwa na ya mataifa mengi ya bara la Afrika kutokana na ukwasi wao unaotokana na kuitumikisha bara letu la Afrika. Si ajabu kuona kuwa mshahara wa anayefanya kazi ya ubawabu Uarabuni au Ughaibuni ni sawa na wa yule anayefanya kazi ya pengine uhasibu katika benki au hata utabibu katika mataifa mengi ya bara la Afrika. Yumkini hii ni moja kati ya sababu ya Waafrika wengi kuhamia Ughaibuni kusaka ajira wakidai kuwa huku kuna *green pasture*, cha kusikitisha ni kwamba licha ya kulipwa mishahara minene huku Uarabuni na hata Ughaibuni wameishia kudhulumiwa mno na waajiri wao."

Sarafina aliendelea kuyatoa machungu aliyokuwa nayo moyoni, "Nadhani nyote mwakumbuka tukio hilo la juzi la kutamausha lililo..." "Gani hilo?" Tukamkatiza Sarafina kwa shauku ya kujua lililofanyika huku tukimkaribia zaidi ili lisitupite hata neno toka kinywani mwake. "Huyo binti mwafrika mwenzetu aliyelazimishwa kuwanyonyesha mbwa kwa kosa la kusingiziwa huku tu Uarabuni," "Maskini binti wa watu! Huo si ni ubahaimu jamani!" nikasema kisha wenzangu wakaunga mkono, "Sana jamani!" Sarafina akaendelea, "Inasemekana kuwa alimtaka kimapenzi mume wa muajiri wake. Adhabu kwake kwa kosa hilo la kusingiziwa ikawa kwamba awanyonyeshe mbwa. Vipi ikahalisi mbwa akanyonye titi la binadamu? Alipokataa, yule muajiri wake mwanamke muarabu akamfyatua risasi akafa." "Alaaniwe yule mwanamke katili!" Sote tukatamka. "Cha kuatua moyo zaidi ni kuwa hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa dhidi ya mwanamke huyo katili. Inasikitisha sana kuona baadhi ya waafrika wenzetu wakija huku kutafuta maisha na hatimaye kurudishwa Afrika kama mizigo." " Yasikitisha sana," nikajibu kwa

mfadhaiko mkubwa. "Hata hivyo pana ajabu kweli nzi kufia kidondani?" Sarafina akauliza. "Hapana kabisa!" sote tukajibu kwa pamoja.

Hii ndiyo hali halisi tangu zamani. Bara la Afrika halijapiga hatua bado katika kusuluhisha tatizo hili. Viongozi ambao wamekuwa na ari ya kusuluhisha tatizo hili wamejaribu kulileta bara letu hadhi yake lakini mwishowe wakafa katika mazingira ya kutatanisha mathalani *Muamar Gaddafi* na wengine wengi. Kwa njia hii utagundua kuwa wazungu hawana nia njema na bara letu la Afrika. Iweje mtu akupe mkopo na kukutoza riba kubwa alafu adai kuwa ana nia njema nawe? Iweje mtu akae katika maabara kutengeneza virusi vinavyoiangamiza bara la Afrika awe mtu mwenye nia njema katika bara letu? Haiwezekani kabisa. Wao ndio watunga mitihani na kisha kutuuzia majibu kwa bei za kuatua moyo. Mwanafalsafa *Napoleon* alisema kuwa watu duniani wanateseka si kwa sababu ya vurugu ya watu wabaya bali kwa sababu ya ukimya wa watu wazuri. Inasikitisha kuwa baadhi ya viongozi wetu hulifumbia macho na kulizibia suala hili mdomo. Heko kwa *Gaddafi* na *Magufuli* ambao abadani hawangeyafumbia madhila haya macho wala kuyazibia midomo.

*Martin Luther King* alisema kuwa tunapaswa kujifunza kuishi pamoja kama ndugu au tuangamie pamoja kama wajinga. Hivyo basi siku zote nilishinda nikiitazamia siku ambayo mataifa yote ya bara la Afrika yataizingatia na kuikumbatia kauli hii. Ambapo maraifa yote ya bara letu la Afrika yataungana na kupinga unyanyasaji wa wazungu kupitia viongozi bora watakaofuata nyayo za watangulizi wao walioonyesha nidhamu katika uongozi. Aidha, nilishinda nikiitazamia siku ambayo wazungu wote watakuwa kama Tom Johnson, ambapo watatambua kwamba rangi ya ngozi ya mtu na asili yake ni pambo tu na si kigezo cha kubaguana. Vilevile natazamia siku ambayo mataifa ya Ughaibuni yatakuwa na nia nzuri kwa mataifa ya bara la Afrika. Ambapo wataunganika na mataifa ya bara la Afrika kupinga ndoa ya jinsia moja badala ya kuitukuza.

*    *    *

Baada ya muda mfupi wa kufanya kazi katika kampuni hiyo, kampuni ilipata umaarufu zaidi kutokana na uchoraji wangu wa kupigiwa mfano. Ulikuwa uchoraji wenye mnato uliowavutia na kuwakosha wengi. Ulikuwa kama sumaku ivutavyo vyuma. Taasisi mbali mbali zikinijia ili niwachoree ramani ya majengo mbalimbali. Hatimaye Tom Jonson alikuwa na pendekezo kwa mkurugenzi mkuu baada ya kutambua utendakazi wangu katika kampuni hiyo. Pendekezo lenyewe lilikuwa kwamba nipandishwe cheo kutokana na utendakazi wangu ulioiinua kampuni kwa kuiongezea kipato pamoja na kuiongezea umaarufu zaidi ila mkubwa wake huyo hakuridhia.

Baadhi ya maneno yake mkurugenzi mkuu niliyosuudika kuyasikia toka afisini mwake akizungumza na naibu wake Tom Johnson yalijipenyeza masikioni mwangu kwa shuruti. Yalikuwa makali kuliko hata wembe,*"It is not possible for a monkey to be given such a position. That is just a refugee from a poor country who has come to beg in our streets. Am not even sure if I was sobber at the time I was employing him in this company. Perhaps I had taken a little bit of alcohol. Such promotions are just meant for the white people only and not black people. Let him be contented with the position he's holding or else..."* Tom Johnson hakuwa na lake tena baada ya kufokewa. Nikamsikia akijibu kwa sauti hafifu mno, *"But why don't you consider him based on his perfomance. All these progress in our campany is due to his vital role in our company and..."* akakatizwa na mkurugenzi mkuu kwa sauti kali, *"Eeish. Stop it, I've said no!"* Ukali huo na msimamo huo wa bosi ***ukamfaradhisha*** Tom Johnson kuridhia methali ya mwenye nguvu mpishe. Kwa mfadhaiko mkubwa akajibu, *"Is okay sir. Am sorry please."*

Tom Johnson aliamua kunimegea angalau tonge la kioja kilichojiri alipojaribu kunipigania mbele ya mkubwa wake. Tayari nilikuwa

nishapata ***mwao*** wa kioja hicho madhali nilikuwa nimesuudika kuyasikia baadhi yacho. Nikamshukuru mno kwa juhudi zake hizo zilizosheheni upendo. Akanihimiza na kunitia moyo niendelee kuitumikia kampuni kwa moyo wangu wote licha ya juhudi zangu kutotambuliwa kabisa na mkurugenzi mkuu, kisa na maana kuwa mimi nilikuwa mtu mweusi. Kioja hicho abadani hakikunivunja moyo madhali hata mshahara nilioupata niliuona mkubwa na ambao ungeniwezesha kufanikisha maendeleo yangu pamoja na ya walionitegemea.

Niliendelea kuitumikia kampuni hiyo kwa bidii za mchwa na upendo mkubwa huku ***nikilimbika*** hela nilizopata ili baadaye nijue cha kufanya kwa kumshirikisha mke wangu Fatuma. Methali kwamba fimbo ya mbali haiui nyoka kamwe haikuniamshia hisia zozote hasi wala mawazo mabaya dhidi yake mke wangu Fatuma licha ya kila mmoja kuwa mbali na mwengine. Maneno ya wafulani kwamba binadamu kamili hawezi kaa mbali na mchumba wake kwa muda mrefu bila kumwendea kinyume binafsi niliyaona kuwa tetesi na fununu tu zisemwazo na wenye midomo ya kusema hata zisizostahili kusemwa. Nikazidi kumpenda Fatuma kwa dhati mno kama mboni ya jicho langu. Hata nilipopata kazi hiyo ya uhandisi yeye ndiye niliyemjulisha wa kwanza kabla ya kuwafahamisha wazee wangu. Akafurahi ghaya kwa bahati hiyo na ***ufanifu*** huo mkubwa uliotuhusu sote.

Baadaye nilimfahamisha sahibu yangu Neema kadhia ya mafanikio yangu hayo. Kwa moyo wake mweupe mithili ya pamba naye akayafurahia mno. Akanieleza kwamba ati ati na wasi wasi zilizokuwa zimemjaa moyoni kutokana na mimi kutopata kazi yenye hadhi na iliyolingana na kisomo changu sasa zilikuwa zimemtoka moyoni. Zikamwacha mwenye furaha na amani kabisa. Kwa jinsi nilivyomtathmini ili nijue namuweka katika kategoria gani ya mabinti, tathmini zangu zilionyesha kuwa Neema alikuwa binti mmoja katika elfu. Mfano wake

haungempata kwa urahisi. Ili umpate, yumkini ingekugharimu muda mrefu na matembezi mapana. Alikuwa binti adibu kabisa. Aidha, kakirimiwa ukwasi wa utu. Laiti ***wafulani*** wangemuiga binti huyo waiongezee dunia ladha ya kupaishi.

# *Sura Ya Nane*

Katika kampuni hiyo nilizikabilisha akili zangu, upendo wangu na moyo wangu wote katika kufanya kazi. Nikifanya kazi hiyo kwa bidii zaidi mithili ya mchwa bila kutarajia pongezi wala hisani ya aina yoyote ile kwa kazi nzuri niliyokuwa nikifanya. Niliridhika na mshahara huo wangu tu nikitahadhari dhidi ya tamaa zilizomuua fisi. Aidha, nilitahadhari mno dhidi ya kumkosea mkurugenzi mkuu kwa njia yoyote ile. Hata zile pongezi za watu walioifurahia kazi yangu sikutamani azisikie hata kidogo. Alikuwa mja aliyeumbiwa husuda na gere za kumtosha, ambaye kamwe hangetamani kumuona mwafrika akiwa na cheo cha juu hususan katika taifa lao na bara lao kwa jumla.

Sikuwa nimethubutu kumwambia Neema lolote kuhusu ***ubahaimu*** wa mkurugenzi mkuu wa kampuni yetu dhidi yangu hadi aliponieleza kadhia ya masaibu yaliyokuwa yakimsibu kule alikokuwa akifanya kazi. Kumbe naye alikuwa kakumbwa na nilichokumbwa nacho. Alinijulisha kuwa wafanyakazi wenzake walimpendekezea mkubwa wao kuwa akampe Neema cheo kutokana na utendakazi wake mzuri ila mkubwa wao akakataa kata kata pendekezo hilo eti kwa kuwa Neema alikuwa mwafrika Nilimhimiza Neema kutovunjwa moyo na hilo naye akanitendea sawia. Kwa njia hiyo nikawa nimemfaa naye akawa amenifaa na hatimaye tukawa tumefaana. Mwishowe sote tukaishia kuendelea kuridhika na nafasi zetu katika kazi tulizokuwa tukizifanya.

Ubaguzi wa mkuregenzi mkuu katika kampuni yetu dhidi ya mtu mweusi uliwaudhi wafanyakazi wengi waafrika. Aidha, ulidhihirika wazi zaidi alipompiga Thomas kalamu baada ya kumsikia Thomas akihoji ni kwanini utendakazi wangu haukutambuliwa naye kabisa. Nikamsikitikia mno Thomas kwa ubaguzi huo wa bosi dhidi yake. Baada ya kuwaza na kuwazua jinsi ya kumsaidia Thomas, niliamua kuzungumza na Tom

Johnson akamuombee msamaha kwa mkubwa wake ila juhudi hizo hazikuzaa matunda kabisa. Bosi alikataa kata kata na baada ya muda mfupi alimuajiri mzungu kuziba pengo hilo la Thomas. Kwa bahati nzuri Thomas aliajiriwa katika kampuni nyingine ya uhandisi baada ya Tom Johnson kumtafutia kazi katika kampuni hiyo. Thomas akamshukuru mno bwana Tom Johnson. Akaungama kuwa sifa nilizokuwa nikimlimbikizia bwana Tom Johnson zilisadifu kabisa.

Visa vya ubaguzi dhidi ya mwafrika vilishuhudiwa katika kila pembe ya Uarabuni na hata Ughaibuni. Waafrika walidhulumiwa mno. Abadani hawakutambuliwa kama binadamu walioumbwa kwa mfano wa Mungu. Waarabu na Wazungu walijiona waliofaa zaidi. Aghalabu ubaguzi huo ukiniamshia ilhamu ya kuwa katika taifa lisilo na ubaguzi. Tamanio hilo likawa linaongezeka siku baada ya siku. Angalau, nisibaguliwe na kunyimwa nafasi mbalimbali kwa sababu ya rangi yangu wala uraia wangu. Lakini si binadamu hubaguliwa popote pale na mtu yeyote yule? Naam! maisha ya kila mja yametawaliwa na ubaguzi wa aina mbalimbali. Hata nchini kwako waweza kubaguliwa. Waweza kubaguliwa ima kijinsia, kitabaka, kimasomo na hata kikabila. Hivi kuna jinsi ambavyo binadamu tunaweza kusaidiana ikiwa tutafanana? Haiwezekani hata kidogo. Lazima watu watofautiane ndipo mambo yafane kwa kusaidiana.

Utofauti wetu hauko kwa madhumuni ya kututenganisha bali kutufanya tugundue kwamba kila mmoja anamhitaji mwenzake ili kufanikisha mambo yake. Asiyejua anamhitaji ajuaye ili naye ajue. Kipofu anamhitaji mwenye uwezo wa kuona ili akaelekezwe vizuri. Hebu wazia ***nakama*** itakayotokea vipofu wakielekezana wenyewe kwa wenyewe! Licha ya kukithiri kwa ubaguzi, sikuwa na budi kuvumilia ili nifanikishe lililonipeleka Uarabuni. Naam! Huko ndiko nilikojipata. Nilistahili kujikunia huko bila kukata tamaa kwa yaliyonisibu. Unyenyekevu wa nyasi ndio niliouchagua kuwa hirizi iliyonikinga dhidi ya maumbufu ya

aina yoyote ile ya watu weupe kama walivyojiita. Laiti wangekuwa weupe wa nyoyo pia waukumbatie utu na kuasi ubahaimu wao huo.

# *Sura Ya Tisa*

Hatimaye nilihisi kwamba hela ambazo tayari nilikuwa nimezilimbika zingenifaa. Lakini zingenifaa tu? La hasha! hazingenifaa tu bali zingenifaa kwa mafao maridhawana. Hela hizo zingetosha kununua shamba huko nyumbani na kujijengea jumba zuri tu tena la kifahari pamoja na kuwajengea pia wazazi wangu nyumba. Aidha, zingemuwezesha mchumba wangu Fatuma kuanzisha biashara ambayo ingemuingizia kiasi kikubwa cha mapato. Lililobakia ilikuwa sasa ni kushauriana na Fatuma kuhusu nia na mipango yangu. Baadaye tungeyatekeleza yale ambayo tungekubaliana.

Baada ya kumpendekezea Fatuma nia na mipango yangu kuhusu jinsi tungetumia hela nilizokuwa nazo, Fatuma hakuwa na lolote wala chochote cha kupinga. Aliridhia kabisa. Kwa kuwa nilikuwa bado kazini Uarabuni, niliamua kumpa jukumu hilo la kutafuta sehemu nzuri ya kununua shamba ambapo tungejenga, kusimamia ujenzi huo pamoja na kuanzisha biashara. Kwa kisomo chake cha uhasibu niliamini kuwa usimamizi wa hela ambazo ningekuwa nikimtumia kufanikishia miradi yetu hiyo hakungempiga chenga hata kidogo. Sisemi kuanzisha na kusimamia biashara ambayo tulipanga kuanzisha. Haya yote angeyaweza na kuyamudu kabisa.

Vile vile sikuwa na hofu kwamba ningedanganywa na mchumba wangu Fatuma kwa lolote. Nilimuamini zaidi madhali hakuwa amewahi kunidanganya tangu tujuane. Niliamini angedumisha uaminifu katika matumizi ya hela hizo na hata wa uhusiano wake nami. Habari za kutamaushwa naye na laiti ningalijua kipindi ningerudi nyumbani barani Afrika abadani sikuzipa nafasi kuwa kati ya niliyoyawazia. Yeye alikuwa mchumba wangu, tena niliyeamini kuwa ananipenda kwa dhati. Kwanini ningekuwa na wasiwasi naye?

Miinukoni lilikuwa ndilo eneo ambalo Fatuma aliniambia kuwa alinunua shamba ekari mbili baada ya kumtumia pesa za kufanikisha zoezi hilo. Ilikuwa eneo nililolifahamu barabara. Halikuwa kitalifa sana na kijiji chetu cha Msonge nilikozaliwa na walikoishi wazazi wangu. Lilikuwa eneo ambalo ukulima wa vyakula mbalimbali ulilikubali kabisa. Mimea mbali mbali katika eneo hili ilikua na kunawiri vizuri. Si mihindi, si ngano, si viazi mbatata, si mihogo, si... Kifupi niseme tu kwamba eneo hilo lilikuwa na uwezo wa kuzalisha vyakula tele vya aina mbalimbali kutokana na mchanga wake wenye rutuba. Watu hawakukosa vya kutia kinywani ije msimu wa mvua ije msimu wa kiangazi. Ndilo lililokuwa eneo lililokimbiliwa na watu wa vitongoji jirani msimu wa kiangazi ulipobisha hodi. Ukwasi wa walioishi Miinukoni ulitokana na uwekezaji wao katika zaraa. Utajiri huo na nyumba za kifahari zilizopatikana katika eneo hilo pamoja na umiliki wa magari ya kifahari na wenyeji wa huko.

Ilisemekana kwamba awali wakoloni waliishi Miinukoni kutokana na mchanga wake wenye rutuba. Enzi hizo waafrika nchini mwao Hawinde walidhalilishwa na kuumbuliwa vya kutosha na wakoloni hao. Wengi walitumikishwa kama punda na fahali mashambani. Kutwa nzima walishinda makondeni wakilima huku wakicharazwa mijeledi migongoni bila imani. Halikadhalika, waafrika hawakuruhusiwa kuishi eneo la Miinukoni na sehemu zingine zenye rutuba. Wao waliishi maeneo ambayo hayakuwa na uwezo wa kuzalisha mimea ya vyakula. Katika eneo hilo, wakoloni walifuga ng'ombe wa maziwa, walipanda ngano, mahindi, maua pamoja na chai na kahawa. Waafrika waliopatikana Miinukoni enzi hizo walikuwa wafanyakazi tu katika maboma na mashamba ya wakoloni hao. Vugu vugu la MAU MAU (Mzungu Arudi Ulaya Mwafrika Apate Uhuru) lilipoanzishwa ndipo waafrika walipoanza kunyakua mashamba katika eneo hilo baada ya wakoloni hao kutimuliwa.

Cha kusikitisha ni kwamba, hata baada ya kuondoka kwa wakoloni hao wazungu bado palisalia Wakoloni weusi. Hawa walijinyakulia mashamba makubwa makubwa bila kuwafikiria waafrika wenzao ambao hawakuwa na hata pa kukanyaga. Ule uhuru ambao waliupigania na hata ukagharimu maisha ya baadhi yao haukuwa na faida hata kidogo kwao. Iweje tuungane kwa nia moja ya kumtimua adui yetu sote na baada ya kufanikiwa kumfurusha adui huyo tuanze tena kudhulumiana wenyewe kwa wenyewe? Iweje mtu umiliki mashamba makubwa makubwa kiwango cha kutojua hata ukubwa wake na mwenzako uliyeshirikiana naye kumtimua adui aishie kuishi katika nyumba ya kupanga miaka nenda miaka rudi eti kisa na maana hana shamba, hawezi hata kulima akajipatie kipato? Kuna haja gani umiliki mashamba hayo yote na ufapo uzikwe katika kijishimo kidogo tu chenye ukubwa wa mita moja kwa mbili?

Tumeruhusu tamaa iliyomuua fisi kutunyima upendo kwa wenzetu. Tusiwaone wenzetu kama wanaofaa pia kumiliki vya kumiliki. Ninaamini iwapo tungeishi kuiandama nadharia ya *Alexander The Great,* basi hatungeruhusu vitu vya kidunia kutukosesha upendo na ujali kwa wenzetu. Mwanafalsafa *Alexander The Great* kwa mtanzamo wake anaona binadamu azaliwapo huwa haji na chochote duniani na hata afapo, vyote alivyovipata duniani huviwacha papa hapa duniani.

Nilifurahishwa mno na hatua ya mke wangu Fatuma kununua shamba Miinukoni. Angalau tungefanya ukulima katika sehemu ambayo ingebaki baada ya kujenga. Baadaye nilimtumia Fatuma hela za kuweka ua aushi katika shamba letu hilo pamoja na za kujenga. Ujenzi wa jumba hilo tulilopania kuwa nalo ulipoanza, Fatuma alikuwa akinifahamisha mara kwa mara ulipofikia. Lililonitia kiwewe kidogo ni hatua ya Fatuma kukataa kunitumia picha za jinsi ujenzi huo ulikuwa ukiendelea. Kila nilipomuomba akapige picha na kunitumia alishinda akiniambia kuwa kazi inaendelea vizuri na nisiwe na tumbo joto hata kidogo. Akiniahidi kuwa

atanitumia picha tu pindi jumba hilo litakapokamilika. Hata hivyo sikuwa na budi kuondoa hofu niliyokuwa nayo baada ya Fatuma kunihakikishia kuwa kila kitu kilikuwa sawa. Lililoniondoa hofu zaidi ni kwamba hakuwa amewahi kunidanganya hata siku moja.

Ukweli kwamba tabia za mtu huwa sawa na rangi ya kinyonga na kwamba hubadilika kulingana na mazingira aliyomo kipindi hicho haukuwa umenipambaukia bayana. Aidha, kupatwa na mtamauko kutokana na kubadilika kwa Fatuma hakukuwahi nipitikia akilini. Siku zote nikishikilia kuwa Fatuma alikuwa bado ndiye yule yule wa juzi, jana na leo kitabia. Binti adibu kabisa. Mawasiliano baina yetu wawili yaliendelea vizuri, kila mara akinijulisha ujenzi ulivyoendelea na ulipofikia. Hata mradi huo ulipokamilika akatimiza alichokuwa ameniahidi awali; akanitumia picha ya jumba alilodai kuwa ndilo alilolisimamia ujenzi wake. Jumba lililokuwa limenigharimu mno kuanzia mwanzo wa ujenzi wake hadi kumalizika kwake. Nilivyoliona kwenye picha alizonitumia, lilikuwa jumba na nusu. Lilikuwa la kuvutia mno.

Nilimpongeza Fatuma zaidi kwa kazi aali aliyoifanya pamoja na uaminifu wake wa kupigiwa mfano. Wasemao husema kuwa mja husadiki pindi aonapo. Niliona nikaamini kuwa hela zangu zilitumika vizuri kwa kunitimizia niliyopania. Nikamuamini zaidi kipenzi changu Fatuma bila ati ati ya nui yoyote.

Baadaye Fatuma alinipendekezea kwamba alitaka kufungua duka la kuuza nguo, viatu pamoja na mapambo mbalimba ya wanawake katika soko la Miinukoni. Aliniambia kwamba baada ya kufanya uchunguzi wake katika soko la Miinukoni, aligundua kwamba hapakuwa na maduka mengi ya kuuza nguo, viatu pamoja na mapambo ya nui mbali mbali. Hali ambayo iliwashurutisha watu wengi wa Miinukoni kuambua nyayo zao hadi masoko ya mbali kutafuta nguo, viatu na hata mapambo

ya mapendeleo yao. Hiyo ilikuwa fursa ya kibiashara aliyoitambua na ambayo alihisi kwamba ingemuingizia kipato kikubwa zaidi.

Nilimsaidia Fatuma kuanzisha biashara hiyo baada ya kumtumia pesa alizozitumia kama mtaji wa kuanzisha biashara hiyo. Kwa jinsi nilivyompenda na kumuenzi Fatuma, nilikuwa radhi kumfanyia lolote alilolitaka kadri ya uwezo niliokuwa nao tena bila wasi wasi wa aina yoyote. Sikutaka akose lolote alilolitaka madhali hilo lingemuondolea furaha na kumuachia karaha. Uso wake uliomeremeta metumetu kama nyota kila alipotabasamu sikutaka kamwe utawaliwe na huzuni hata kidogo. Nilitaka ashinde akitabasamu usiku kucha na mchana kutwa. Nilipania mchumba bora zaidi kwake ambaye badala yangu hangempata popote pale.

Niliumithilisha uso wake Fatuma na ua la waridi upendezao mno wakati wa asubuhi na ambao hunyauka kutokana na dhuluma za jua kali la kutwa nzima. Hivyo nilijitahidi nisiwe kama jua kali la kutwa nzima ambalo lingeudhulumu uso wake kwa kuunyausha. Nia yangu ilikuwa ni kumpigisha Fatuma mbizi katika bahari ya mapenzi maridhawa. Nilimuona kama zawadi niliyokirimiwa na Karima na hivyo basi sikuwa na budi kumpenda kwa dhati na kumuwajibikia ipasavyo. Kabisa sikutaka kuwa katika orodha ya wale wakosao kuthamini walivyozawadiwa na baadaye wakapokonywa na kujutia mapuuza yao.

# *Sura Ya Kumi*

Kangaja kangaja ambayo baadaye huenda yakaja hatimaye yalikuja. Baada tu ya kumtumia Fatuma pesa alizodai alitaka kuzitumia kama mtaji wa kuanzishia biashara, Fatuma alianza kupunguza mazungumzo nami. Kila nilipompigia simu, simu yangu ingeita bila kupokelewa na hata baadaye iwapo angepata ***simu fifi*** yangu hangethubutu kunipigia ajue nilimpigia kwanini. Mara chache nilizosuudika kuzungumza naye, nilishinda nikimuuliza kwanini aliondokea kupunguza mazungumzo nami kiasi hicho madhali nilihisi kwamba lazima kulikuwa na jambo ambalo halikuwa sawa.

Majibu aliyonipa Fatuma abadani hayakuuridhisha moyo wangu uliokuwa ukivuja damu. Moyo ambao kwa wakati huo haukuwa na amani kabisa. Mara kwa mara akinijibu kwamba shughuli za kibiashara ndizo zilizomnyima muda wa kuzungumza nami. Iliniwia vigumu sana kutozungumza na niliyemfanya mboni ya jicho langu. Mazungumzo ya mara kwa mara na Fatuma yaliyokuwepo hapo awali sasa hayakuwepo tena. Nilijiona samaki aliyetolewa majini na kutupwa katika nchi kavu. Sehemu yenye uhaba wa maji. Tena maji ambayo yangenihakikishia uhai. Sasa yangepita hata majuma mawili ndipo nisuudike kuzungumza na Fatuma. Yeye hangethubutu kunipigia simu hadi mimi mwenyewe nikampigie. Endapo singempigia basi mawasiliano baina yetu hayangekuwepo.

Hata kila nilipompigia na kuzungumza naye hakuwa yule Fatuma niliyemjua na kumzowea tena. Ule uchangamfu aliokuwa nao mwanzoni haukuwepo tena. Sisemi maneno matamu matamu yaliyoipiku asali aliyokuwa akinitamkia kama mwandani wake kabla ya kulala na kila nilipoamka. Hizo zilikuwa dalili za mvua ambazo sasa nilikuwa nimeshaanza kuziona. Ilinibidi sasa niwe mstahimilivu ningojee mvua

kunya. Kila nilipomuuliza tatizo lililokuwa likimsumbua, alishinda akiniambia kuwa hapakuwa  na tatizo lolote lililokuwa likimsumbua. Nikamuona Fatuma kama muwele. Tena muwele ambaye ugonjwa wake haukujulikana sembuse kuutibu? Kwa kawaida ugunduzi wa aina ya ugonjwa umtaabishao mgonjwa husaidia pakubwa katika kupata tiba mwafaka. Huwa ndio hatua ya kwanza ya upataji suluhu kwa ugonjwa wowote ule. Ni muhali mno kupata tiba ya ugonjwa ambao haujajulikana. Sikupata amani kabisa kwa mbadiliko huo wa Fatuma wa ghafla. Hapo ndipo nilipoungama kwamba mazowea yana tabu yake.

Hata kazini wafanyakazi wenzangu walionijua vizuri kama Sarafina walitambua kwamba hali yangu haikuwa ya kawaida. " Ndugu Yohana kwanini hauko mchangamfu kama kawaida? Siku hizi nakuona mnyamavu zaidi, hauna furaha na hata maneno toka kinywani mwako twayasikia kwa tukizi mno! Nadhani lazima kuna jambo linalokuvuruga mtima. Hebu niambie!" Akasihi Sarafina huku akiungwa mkono na wengine, "Naam, tuambie. Tuko radhi kukusaidia ndugu."  "Jambo tu ninaloweza kuwaambia kwamba lanisumbua ni kwamba hakuna linalonisumbua. Mie niko sawa kabisa na wala msiwe na hofu nami." Nikawajibu na kisha wakaangua cheko kubwa kwa jibu langu hilo.

Siku zote niliitikadi kwamba kuna mambo yanayokuhusu wewe mwenyewe ambayo hata sahibu wako wa ndani zaidi hapaswi kujua. Kuna watu ambao wanapojua baadhi ya mambo yako huyatumia kama silaha ya kukuangamizia. Wao hukushawishi na kukupumbaza hadi uwaambie siri zako kwa dhana ya kukusaidia lakini baadaye badala ya kukusaidia wao huondokea kukutilia msumari moto kwenye kidonda chako hicho. Hata sahibu yangu Neema sikuthubutu kumhusisha kwa njia yoyote ile. Sikutaka kuishi kabisa nje ya sera yangu hiyo niliyoiandama siku zote. Yaliyokuwa yakinikabili niliamini kuwa vilikuwa vita ambavyo

ningepigana navyo mwenyewe na hatimaye nivishinde. Sikutaka msaada wa mtu yeyote katika hilo.

Kutozungumza na mke wangu Fatuma mara kwa mara kama nilivyozowea hapo awali kulinipa tabu mno. Aidha, nilihisi kuwa hapakuwa na tabu iliyozidi tabu hiyo. Ilinibidi niiridhie hali hiyo geni ambayo sikuwa nimeizowea hata kidogo. Hali niliyoiona kuwa ya upweke na ukiwa uliopitiliza. Wasemao husema kuwa muda ni dawa mujarabu wa vitushi vya maisha. Niliamua kuupa muda jukumu la kunieleza kinagaubaga yaliyokuwa yakiendelea bila utambuzi wangu. Muda ukawa silaha niliyoichagua na kuiona ya kufaa zaidi katika vita hivyo nilivyokuwa nikipigana navyo. Nilikuwa na uhakika kwamba muda ungenipa ushindi usiopingika.

Niliendelea na kazi yangu katika kampuni hiyo ya uhandisi huku shauku ya kutaka kurudi nyumbani barani Afrika ikiongezeka kila uchao. Nilitamani nimalize mkataba wangu huo niende nyumbani nikae karibu na mchumba wangu Fatuma na kuishi naye. Aidha, iwe fursa ya kukitegua kitendawili kilichokuwa kikinisumbua kwa siku ayami tangu nilipoanza kuhisi kwamba lazima kulikuwa na doa katika uhusiano wetu au pengine ndoa yetu.

Hatimaye niliamua kubuni njia mpya ya kuzungumza na Fatuma mke wangu baada ya yeye kuyapunguza mawasiliano yetu zaidi. Kumtumia jumbe za salamu na heri za mara kwa mara ndiyo iliyokuwa njia yangu mpya ya kuzungumza naye. Lolote nililokuwa nalo moyoni nilimpasha kupitia jumbe hizo. Maskini nilishinda nikimtumia jumbe hizo hata bila ya kupata majibu toka kwake. Sikutaka kujua namna alivyozipokea jumbe hizo, alimuradi tu zilimfikia. Daima nikijifarijisha kwamba huenda jumbe hizo zingekuwa na athari ya kumkumbushia jambo alilokuwa labda amelisahau kuhusu uhusiano wetu lakini hilo halikuwahi tokea.

Nilianza kuhisi kwamba nilikuwa fimbo ya mbali kwa Fatuma ambayo kamwe haingeweza kumuua nyoka. Nikaamua kumjulisha kwamba ninapanga kurejea nyumbani baada ya miezi michache kupitia ujumbe huu niliomtumia kwa njia ya barua pepe:

*Kwa mke wangu Fatuma,*

*Hujambo barafu wa moyo wangu? Mie huku niliko sijambo. Uliko kwema kweli? Mbona umekawia kunitumia hata neno tu? Kwaniumiza kunyamaza kwako huku. Usono siupati. Ninatawaliwa na wasiwasi kutwa nzima na hata usiku mzima. Amani imenikimbia. Nimebaini kwamba mazowea kweli yana tabu yake. Tena tabu tumbi nzima. Uraibu wangu kwako wanipa tabu mno. Laiti singekuwa nimezowea kusema nawe mara kwa mara. Naumia sana mpenzi. Lengo hasa la kukuandikia waraka huu ni kukujulisha kwamba baada ya miezi mitatu nitakuwa natua katika uwanja wa ndege wa Vijiweni. Naja tuishi pamoja raha mustarehe, tuondoane upweke na ukiwa. Nitakujulisha tarehe kamili ya ujio wangu uje unilaki pale uwanjani. Nakupenda zaidi ya unavyodhani mpenzi wangu. Shukrani!*

*Wako wa mtimani,*

*Mstahimilivu Yohana.*

Nilitamaushwa na kuatuliwa moyo na hatua ya Fatuma kutonijibu lolote hata baada ya kuupokea ujumbe huu. Hakudiriki kunijibu hata kwa neno moja tu. Hali hiyo ilinizidishia ari na ghera ya kwenda nyumbani hata kabla ya kukamilisha mkataba wangu katika kampuni hiyo ya uhandisi nilimokuwa nikifanya kazi. Amani ilizidi kunitelekeza kila uchao.

Mtagusano wangu wa mara kwa mara na Peter niliyeishi naye katika boma la Tom Johnson ulimfanya agundue hali yangu hiyo ambayo haikuwa ya kawaida kulingana na alivyonizowea. Yeye alikuwa bado

anafanya kazi katika boma hilo la Tom Johnson. Aghalabu Peter alishinda akinidadisidadisi ili atambue lililokuwa likinisumbua.

Jioni moja baada ya kutoka kazini, Peter alinipata nimeketi barazani mwa jumba la Tom Johnson nikiwa nimezama katika bahari ya luja na kuniuliza, " Ndugu Yohana! Hivi uko sawa kweli? Siku hizi unanyamaza sana. Nahisi kwamba huu ukimya wako wa siku hizi lazima kuna jambo ambalo umelisitiri. Nini linakusumbua?" Nilisafisha koo na kisha nikajibu, "Hamna linalonisumbua Ndugu Peter. Ni uchovu tu wa kazini." "Sidhani kama ni uchovu tu, mimi ninahisi kwamba lazima kuna jambo. Huu ukimya wako wa kila siku umepitiliza sasa." Peter akakanusha kisha nami nikaendelea kuutetea upande wangu, "Mimi kuwa kimya hakumaanishi kwamba ninasumbiliwa na jambo. Kuna nyakati ambazo ni sahihi kabisa kuuziba mdomo wako kuliko kuufungua na kuyatamka hata yasiyofaa. Hivi hujui kuwa samaki aliyefumba mdomo wake ni vigumu mno anaswe kwenye ndoana?" "Unajua kujitetea wewe! Lakini tambua kwamba unaponyamazia shida wewe mwenyewe hatimaye huondokea kuwa shida." Peter akasema huku akiondoka na kuniwacha pale barazani nikitazama runinga.

Hata runinga yenyewe sikuimakinikia sana madhali nilishinda nikitafakari alichoniambia Peter. "Eti ukinyamazia shida hatimaye wewe mwenyewe huondokea kuwa shida" nilijiwazia maneno haya nafsini pale barazani, nikijaribu kufasiri alichomaanisha Peter.

Hata hivyo juhudi hizo za Peter hazikumzalia matunda hata baada ya kutumia mbinu mbalimbali za kutambua lililokuwa likinisibu. Nilishinda nikimpa jibu hilo hilo tu ambalo asilani halikumsadikisha kuwa hapakuwa na lolote lililonisibu.

# Sura Ya Kumi na Moja

Baada ya mpito wa miezi miwili hivi, Peter aliwahi kurudi nyumbani kwao kutokana na mauko ya babake mzazi. Hilo likawa tukio lililomtibulia mipango yake. Akafaradhika kwenda nyumbani kabla ya muda aliokuwa amepanga. Tukio hilo lilimsononesha mno Peter. Kipindi hicho cha majonzi kikamjulisha kuwa kumbe maisha ni mshumaa usiokuwa na mkesha. Wengine husema kuwa maisha ni moshi ufukao kwenda juu angani na ambao huwa hauna marejeo. Alilitambua hili tena kwa uchungu mkubwa. Akahisi kwamba hapakuwa na uchungu mwingine uliozidi uchungu wa kuondokewa na baba mzazi. Nikamhurumia na kumsikitikia mno Peter kwa mauko hayo ya babake.

Kuondoka kwake Peter kukaniwachia upweke usiosemeka. Katika boma hilo la Tom Johnson hapakuwa na mtu mwengine ambaye ningepiga naye gumzo na kusahaulishiana naye dhiki za kibinafsi ambazo kila mmoja angekuwa akiandamwa nazo kisirisiri. Kwa kawaida hapana mja yeyote duniani ambaye hana dhiki maishani mwake. Usishangae kugundua kwamba hata mtoto mdogo azaliwaye sasa ana dhiki zake. Tena dhiki tele mno. Yeye hawezi kujifanikishia mambo yake binafsi bila kumtegemea mamake au babake, mathalani kula, kuoga au hata kujieleza. Kwa yeyote aishiye, lazima awe na tatizo ambalo ima anaweza kuwahusisha wengine kulitatua au yeye mwenyewe kulikabili kisirisiri bila kuwahusisha wenziwe. Asiye na dhiki wala doa sijawahi kumuona. Katika boma hilo la Tom Johnson kulikuwa na mjakazi mwengine aliyefanya kazi za ndani. Yeye hakuwa mbaraza sana, mara kwa mara alishinda peke yake akijishughulisha na yaliyomhusu tu. Hakuwa na muda wa kutangamana na yeyote kati yangu na Peter hadi Peter alipoondoka. Bi. Huruma na mumewe Tom Johnson walionekana katika boma lao kwa tukizi mno kutokana na pilikapilika zao zilizowanyima muda wa kutulia nyumbani mwao.

Hali hiyo ya upweke katika boma hilo iliponielemea, niliamua kumjulisha Bi.Huruma na Bw. Tom Johnson kwamba nilitaka kuondoka nirudi nyumbani ila hawakuridhia. Wakanipendekezea kuwa ni heri niwe mstahimilivu hadi mkataba wangu wa kufanya kazi ukamilike. Sikuwa na budi kustahimili upweke huo hadi muda wa kufanya kazi katika kampuni hiyo ya uhandisi ukamilike. Nilipomuuliza Neema endapo naye alikuwa na mpango wa kurudi nyumbani karibuni akanijulisha kwamba haukuwa na mpango huo. Kwamba alitaka akamilishe mradi wa ujenzi wa nyumba za kupanga aliokuwa ameuanzisha kule nyumbani kwa usaidizi wa kaka yake aliyekuwa akiusimamia ujenzi huo. Nilipomuambia kwamba mimi nilikuwa na mpango wa kwenda nyumbani karibuni akatamani twende sote ila nikamshauri kwamba ilikuwa verma aukamilishe mradi wake huo kwanza. Tukakubaliana kukutana pindi arudipo nyumbani Mungu akiridhia.

Siku ziligeuka wiki nazo wiki zikageuka mwezi. Hatimaye mkataba wangu ukakamilika. Wakati wa kurudi kiamboni ukawa sasa umewadia. Nikajaribu kumtafuta Fatuma kwa simu nisimpate. Nilitaka nimfahamishe tarehe kamili ya kutua katika uwanja wa ndege wa Vijiweni ili aje anilaki pale uwanjani. Hata nilipojaribu kumtumia ujumbe, ujumbe wangu huo haukujibiwa. Nikahisi kuwa pengine alikuwa kaaribikiwa na simu na ndio maana hakuwa anapatikana kila nilipompigia.

Ilibidi nibadilishe ratiba yangu sasa pindi nituapo nchini kwetu salama salimini kutokana na Fatuma kutopatikana hewani. Awali nilikuwa nimepanga kwamba pindi nikutanapo na Fatuma ajapo kunilaki katika uwanja wa ndege tungefululiza pamoja hadi Miinukoni tulikonunua shamba na kujenga. Kutokana na hali hiyo, sasa ilinibidi niwe mnyumbufu zaidi. Nikafanya mabadiliko katika ratiba yangu hiyo ya awali na kuamua kwenda moja kwa moja hadi nyumbani kwetu nikawaone wazee wangu kwanza.

Siku ya safari yangu ilipofika, Bi. Huruma na mumewe hawakutaka nisafiri kwa kuhofia upweke uliokuwa ukiwakodolea macho. Walitaka niendelee kukaa nao katika boma lao hilo hali nikiendelee na kazi yangu. Wakajitahidi kunishawishi ili niendelee kukaa nao ila shauku ya kutaka kufika nyumbani haikuniruhusu hata kusikiliza vishawishi vyao hivyo. Sikutetereka kabisa katika uamuzi wangu huo. Hata hivyo baada ya kuwaelezea sababu zilizonifanya nisitetereke katika uamuzi wangu huo wa kwenda nyumbani, hatimaye walikubali ijapokuwa shingo upande.

Bw. Tom Johnson na mkewe Bi. Huruma wakanisindikiza hadi katika uwanja wa ndege. Wakanilipia nauli pamoja na kunifaa kwa masrufu. Mtu na mkewe walikuwa wakwasi wa utu wema kabisa. Ukarimu wao siku zote ulinishangaza mno na kuniwacha kinywa wazi. Pale uwanjani tukakumbatiana huku machozi yakinichirizika kutokana na utengano uliokuwa ushabisha hodi sasa tayari kuingia kwa shuruti. Wakanitakia heri ya safari na michakato yote ya halafu katika maisha yangu. Nikaahidi kuwajulia hali mara kwa mara kupitia simu pomoja na kuwatembelea siku za usoni. Moyoni nilihisi uchungu mno kutokana na utengana huo. Hata nilipokuwa nikiingia ndegeni, nilisita kidogo na kuwaangalia kwa jitimai huku nikiwapungia mkono wa kwaheri bila kuwaona barabara. Machozi yaliyojitawalia kwenye macho yangu na uso wangu yalinizuia nisiwaone vizuri.

Anga tulivu ya macheo hiyo ilinihakikishia safari njema kabisa. Kabla ya kupaa angani kwa ndege niliuzamisha uso wangu katika vitanga vyangu. Nikamuomba Mungu anijalie na kuwajalia wote waliokuwa katika ndege hiyo safari njema kama ilivyokuwa ada kwangu. Mawingu yalikuwa meupe pepepe kama pamba na kuifanya njia yetu ya angani kuwa shwari. Katika safari hiyo, wengi walikuwa waafrika ambao walishinda wakihadithiana waliyokumbana nayo Uarabuni. Wengine wakila yamini kutorudi huko tena kutokana na masaibu yaliyowasibu kule Uarabuni.

Aidha, wengine walijilalia usingizi wa pono. Nadhani kutokana na uchovu wa kazi nyingi walizoshinda wakizifanya katika maboma ya Waarabu kutwa nzima na usiku kucha. Wengi hawakupata muda wa kutosha kupumzika. Walitumikishwa hata zaidi ya punda. Baada ya saa kumi za safari, hatimaye ndege ilitua katika uwanja wa Vijiweni. Nikamshukuru Mungu kwa safari hiyo ambayo haikuandamwa na dosari ya aina yoyote. Baada ya kushuka nikahisi badiliko la tabia nchi; kiwango cha joto kilikuwa juu ikilinganishwa na cha Uarabuni.

Pale uwanjani kulikuwa na halaiki kubwa ya watu waliofika kuwalaki wandani wao. Walionekana wakipigana pambajana kwa furaha isiyo na kifani na wandani wao waliokuja kuwalaki. Wengine walichirizikwa na machozi ya furaha kutokana na furaha ya kukutana tena na wendani wao baada ya muda mrefu. Mimi ambaye sikuwa na wa kunilaki nilishinda nikiwatumbulia macho tu kwa husuda. Niliamua kuingiza mkono mfukoni mwa suruali yangu ndefu na kuchomoa simu yangu ya mkononi ili nimpigie tena Fatuma. Nikidhani kwamba huenda angeipokea simu yangu. Maskini baada ya kumpigia hakuwa anapatikana hewani tena. Hali hiyo ikanimalizia nguvu miguuni na mikononi. Ikaniwacha hoi kabisa. Simu yangu hiyo niliyokuwa nimeiweka sikioni kwa mkono wangu wa kuume ikajiagukia chini kwa imani kubwa bila hata ya ufahamu wangu.

Nilimuwazia Fatuma nikaishia kudondokwa na machozi kutokana na fundo chungu nililolihisi. Kadhalika niliwazia na kujichorea taswira ya jinsi hali ingekuwa endapo angefika kunilaki pale uwanjani. Tungekumbatiana kwa furaha isiyo na mfanowe. Sikuwa na budi kumeza mate machungu ambayo hata karibu yanisakame na kujiondokea upesiupesi bila kuangalia nyuma. Nilihisi kuwa iwapo ningeendelea kutazama jinsi watu walivyofurahiana pale uwanjani ningeendelea kuumia zaidi. Ingekuwa sawa na kujitilia msumari moto kidondani.

Nilienda moja kwa moja hadi katika stendi ya magari machweo hiyo iliyotawaliwa na utusi utusi kutokana na giza iliyokuwa imeanza kuingia. Hapo nikapanda basi la kwenda Msonge kiamboni kwetu. Katika safari hiyo ya usiku, usingizi haukudiriki kunishika licha ya uchovu wote huo wa kutwa nzima. Yamkini hali hiyo ilitokana na msongo wa mawazo yaliyojitawalia kichwani mwangu. Katika safari nzima macho yangu hayakulegezwa hata kidogo na usingizi ulionikimbia. Nilikuwa amilifu kabisa huku magurudumu ya basi hilo yakichuana na barabara usiku kucha. Uamilifu wangu huo ukaniwezesha kuona vibandiko viwili vya rangi nyeupe vilivyonatishwa ndani ya basi hilo. Kibandiko cha kwanza kilikuwa kimenatishwa karibu na dirisha lililokuwa karibu nami. Nacho kilikuwa na maandishi haya yaliyokolezwa kwa rangi nyekundu; ***Ukimwamini mtu sana utatamauka***. Hicho cha pili kilikuwa kimenatishwa kwenye mlango wa basi hilo. Nacho kilikuwa na maandishi haya yaliyokolezwa kwa rangi nyekundu sawia na hicho cha kwanza; ***Kitambi na mimba ni bidii ya mwanaume.*** Alimuradi kila kibandiko kilikuwa na ujumbe wa kuwasilisha kwa waliowahi na tuliokuwa tukiabiri basi hilo wakati huo.

Ujumbe uliopitishwa kwenye kibandiko hicho cha pili *ulinitabasamisha* mno. Nafsini nikashinda nikijichekea hadi nilipoanza kufasiri maandishi yaliyokuwa kwenye kibandiko cha kwanza eti *Ukimwamini mtu sana utatamauka.* Mantiki ya maandishi hayo yalikuwa ya moja kwa moja tu. Sikuhitaji kujikuna kichwa ili nipate ujumbe wake au pengine maana yake madhali ulikuwa sawia na kitendawili chepesi ambacho hata mtoto wa darasa la chekechea angekitegua kwa ***usahali*** mno. "Je, inawezekana nikapatwa na mtamauko baada ya kumwamini sana mchumba wangu Fatuma? Haiwezekani! Naam, haiwezekani.Yeye tangu tuanze uchumba wetu hajawahi kunidanganya wala kunisaliti hata siku moja kwa njia yoyote ile. Hata hivyo si watu hubadilika kitabia kutokana na mpito wa wakati na mazingira waliyomo. Leo ni mkweli kesho ni

muongo, leo mkarimu kesho mchoyo. Naam, sisi binadamu tabia zetu ni sawa na rangi za kinyonga tu. Hubadilika kulingana na mazingira tuliyomo. Potelea pote, haiwezekani!"  nikajiwazia nafsini.

Nilijitahidi kutoruhusu ujumbe huo na makisio yangu hayo yaninyime utulivu wa moyoni baada ya kuuwazia ujumbe huo na kuuhusisha na Fatuma ila nikashindwa. Nikasadiki kwamba ni muhali sana kupingana na hisia ambazo huwa hazifichiki. Hata ile tabasamu iliyochochewa na ujumbe wa kibandiko hicho cha pili ikanitoweka ghafla usoni.

# *Sura Ya Kumi na Mbili*

Nilipofika nyumbani ilikuwa ni saa moja za asubuhi. Wazee wangu walikuwa tayari washaamkia hamsini zao za siku hiyo. Walikuja kunilaki pale getini kwa bashasha isiyomithilika. Pale getini tukapigana pambaja kwa furaha mpwitompwito kutokana na utengano wa muda mrefu. Ama kweli tulikuwa ***tumepezana*** vya kutosha. Hatimaye tulifululiza hadi barazani mwa jumba nililokuwa nimewajengea.

Pale barazani mama alitandika meza kwa chai, vitumbua na karanga. Tukanywa chai hiyo kwa vitumbua na karanga pamoja. Nilifurahi ghaya ya kufurahi kushiriki staftahi hiyo pamoja na wazazi wangu baada ya muda mrefu. "Karibu sana mwanangu. Pole kwa uchovu wa safari ndefu." akatanguliza mama na kuufukuzilia

mbali ukimya uliokuwa umetawala. "Ahsante sana mama," nikajibu. "Vipi mwenzio, umemwacha wapi?" Akauliza baba. Swali lake baba likawa chanzo cha mjadala na mazungumzo yaliyodumu kwa muda mrefu siku hiyo “Nani tena baba?" Nami n'kauliza kwa mshangao. "Mwanangu jamani, yani unataka kutuambia haumjui mkeo Fatuma?" Akauliza mama kwa upole. "Hivi unamaanisha kwamba hukumtumia Fatuma nauli za kuja Uarabuni huko unakotoka?" Akauliza tena baba. "Sijawahi wasiliana na Fatuma kuhusu suala la yeye kuja kule Uarabuni. Hela nilizomtumia zilikuwa za kufanikishia mradi wetu wa kununua shamba kule Miinukoni pamoja na ujenzi wa nyumba!" Nikajibu. Kadri nilivyozidi kuulizwa maswali hayo ndivyo nilivyozidi kuchanganyikiwa zaidi. Hata ile chai ikawa haina ladha tena iliyokuwa nayo hapo mwanzoni.

Wazee wangu nao walikuwa katika hali sawia na yangu. Walishangazwa sana kwa jibu langu lililooonyesha bayana kuwa sikuwa nimekutana na Fatuma kama walivyodhani. Niliendelea kuwaelezea, "Hatimaye nilimtumia Fatuma hela za kuanzishia biashara kama alivyodai

ila tu baada ya kumtumia hela hizo akapunguza mazungumzo nami kabisa. Kila nilipompigia simu hakuwa akipokea simu yangu na hata mara chache alizowahi kupokea, hakuwa akinipa muda wa kutosha wa kuzungumza naye. Aghalabu alidai kuwa shughuli za biashara aliyoanzisha ndizo zilizomnyima muda wa kuzungumza nami." Nilisita kidogo katika mchakato wa kushusha pumzi na kisha nikaendelea, "Kinachonikosesha amani zaidi ni kwamba hapatikani kwa simu kabisa. Hakuna mawasiliano yoyote yanayoendelea kati yangu naye. Hata pindi nilipotua tu nchini jana jioni na kujaribu kumtafuta kwa simu akawa hapatikani kabisa. Nahisi kwamba Fatuma amenikatia mawasiliano. Lazima kuna jambo ambalo haliko sawa kabisa!"

"Inasikitisha sana! Fatuma alipotoka hapa nyumbani alituambia kwamba umemtumia nauli aje kule Uarabuni. Tulipotaka kumsindikiza hadi katika uwanja wa ndege akasema hapakuwa na haja. Mimi na babako tukawa hatuna budi kuridhia alivyotaka yeye. Tukamtakia heri ya safari njema tukijua kwamba anakuja huko kukutembelea ila tunashangaa kwamba alikuwa anatudanganya tu!" Akasema mama kwa masikitiko makubwa. "Ama kweli mahusiano yenu haya na ndoa zenu hizi za siku hizi ni mchezo wa karata tu," naye baba akasema kwa ghadhabu. Nilishangaa na kushtuka mno kutokana na alichosema mama. Kuamini kwamba Fatuma angeweza kuwaongopea wazazi wangu kukawa nje ya uwezo wangu; Sikuamini kabisa. Uchovu niliokuwa nao pamoja na hali hiyo vyote vikachanga bia kunifanya niwe hoi kabisa. Nafsini nikajiuliza maswali mengi yaliyohusu kadhia hiyo bila kupata majibu yake.

"Tangu aondoke hapa amewahi kuwasiliana nanyi?" Nikauliza. "Hapana mwanangu. Hajawahi kutupigia simu wala kututumia ujumbe wowote. Matarajio yetu kwamba angetufahamisha kuhusu safari yake pindi afikapo Uarabuni yalikuwa sawa na kutarajia kuku abahue. Kila mara tulipomtafuta kwa simu alikuwa hapatikani. Mara nyingine tulihisi

kwamba huenda kutopatikana kwake kulisababishwa na mkinzano wa mtandao wa nchini kwetu hapa na wa kule Uarabuni." Akasema mamangu. "Wewe nenda Miinukoni kesho ukakutane naye ana kwa ana. Nadhani yuko kule. Ukazungumze naye ujue ni kipi kinachomfanya asizungumze nawe na hata sisi wakwe zake. Hata hivyo hatujui ni eneo lipi hasa la Miinukoni alikonunua na kujenga. Iwapo kungekuwa na mawasiliano kati yetu naye basi inawezekana hata tungekuwa tumemtembelea katika boma lenu hilo." Akapendekeza baba. Mama naye akaunga mkono, "Naam, itakuwa jambo zuri ukizungumza naye. Sisi tuko radhi kumsamehe kwa kutotuambia ukweli. Hatuna kinyongo naye." "Ni sawa wazee wangu. Naomba nikapumzike kisha kesho nifike huko kama mlivyoniagiza na nilivyokuwa nimepanga pia." Nikaridhia mapendekezo yao ambayo hayakukinzana na niliyokuwa nimepanga. Baadaye nikaingia katika chumba alichokuwa ameniandalia mama kupumzika.

Siku iliyofuata niliwahi Miinukoni nikiwa na hamu kubwa ya kukutana na mchumba wangu Fatuma. Vile vile nilikuwa na hamu ya kufika kule ili nione boma langu hilo. Juhudi zangu za kumsaka Fatuma kwa simu zilikuwa zimeambulia patupu kabisa. Awali Fatuma alikuwa amenieleza eneo kamili pale Miinukoni alikonunua shamba na kujenga. Kadhalika, kwa maelezo yake hayo, aliniambia kwamba eneo hilo lilikuwa karibu kabisa na shule ya msingi ya Miinukoni. Kwa kufuata maelezo yake hayo, nilienda moja kwa moja hadi eneo hilo. Nilipofika eneo hilo, nilianza kumuuliza kila mmoja aliyeishi eneo hilo iwapo kuna yule aliyemfahamu Fatuma. Kila niliyemuuliza aliniambia kwamba hakuwa anamfahamu. Kwa muonekano wa eneo hilo, hapakuwa na hata nyumba moja iliyokuwa mpya. Nyumba nyingi zilikuwa zenye mabati machakavu kabisa. Mabati yaliyodhulumiwa na kutu kwa muda mrefu.

Nilitamauka kwa kutoona nyumba yoyote iliyolandana na ile picha ya nyumba aliyowahi kunitumia Fatuma. Nyumba ambayo alisimamia

ujenzi wake na iliyonigharimu vya kutosha. Hata baada ya kutembea maeneo yote ya Miinukoni, sikusuudika kumpata yeyote aliyemfahamu Fatuma au aliyefahamu alikokuwa akistakimu. Sikubahatika pia kuona nyumba yoyote iliyolandana na hiyo aliyowahi kunitumia picha yake. Hali hiyo ilinipa kiwewe mno. Nikatamani Fatuma angepatikana hewani anirahisishie kibarua hicho kigumu. Aidha, aniondolee hofu niliyokuwa nayo moyoni. Hakuna rafiki yake hata mmoja niliyekuwa na nambari yake ya simu, pengine ningempigia nimuulize iwapo alijua alikokuwa akiishi Fatuma. Sikutaka kuendelea kuwa mfungwa huru tena. Nilikuwa radhi kujitolea kwa hali na mali kufanya lolote alimuradi liniondolee tatizo hilo lililoninyanyasa nikanyanyasika shibe yangu. Nilitaka niwe huru kabisa kama waja wengine na wala si wafungwa walioishi daima dahari kuteseka ulimwenguni.

Baada ya mahangaiko hayo ya kutwa nzima bila ya mafanikio, niliamua kurudi nyumbani nikiwa mchovu na dhaifu sana. Upepo tu ungetosha kunibwaga chini. Mawazo tele yaliyojitawalia akilini mwangu yalinifanya nihisi kama kwamba nilikuwa nimeubeba mzigo mzito mithili ya nanga kichwani. Mishipa ya kichwani nayo ilijitokeza wazi wazi kabisa. Macho yangu nayo yalikuwa mekundu ungedhani moto ya jehanamuni. Haingemwia vigumu yeyote aliyeniangalia na kuniona barabara kutambua kwamba hali yangu haikuwa shwari. Angetambua kwa usahali mno kwamba shari ilikuwa kivuli kilichoniandama kwa shuruti.

Nilipofika nyumbani, niliwapata wazee wangu wakiwa tayari kupata ripoti kuhusu mambo yalivyokuwa kutwa hiyo. Nilipowaeleza kwamba sikufanikiwa kukutana na mchumba wangu Fatuma na wala hakuna yeyote aliyemfahamu katika eneo hilo hata baada ya kumuuliza kila mmoja aliyeishi eneo hilo, walitamauka mno kwa ripoti hiyo ya kuvunja moyo. Wakanisikitikia mno kwa juhudi zangu zilizoondokea kuwa tasa. Mama alipojitahidi kuhimili machozi ambayo wafulani husema

kuwa yaliumbiwa makoo tu na wala si majogoo alishindwa. Binafsi niliamini kwamba hata wanaume wanafaa kulia wakabiliwapo na masaibu ili waweze kuishi muda mrefu. Kunyamazia uchungu moyoni bila kuutoa nje kwa njia ya machozi ni kujilimbikizia ndwele hatari ambazo tiba zake hugharimu mno. Wakati mwingine hugharimu hata maisha ya mtu. Zipo nyakati ambazo machozi huwa dawa mujarabu ya kuondoa machungu ya mtimani.

Uchungu wa mwana ambao aujuaye ni mama tu ulidhihirika bayana kupitia kilio cha mama kwa yaliyonisibu. Mama aliufanya uchungu wangu huo kuwa wake. Akalia sana kutokana na dhiki hiyo iliyonisibu. Nilijitahidi kumpembeja kwa kumtia moyo kwamba mambo yangu yangekuwa sawa tu hadi alipotulia na kuikubali hali hiyo na vile vile kuridhia kwamba hali hatimaye ingekuwa shwari.

Hatimaye nilijiwa na wazo. Wazo lenyewe lilikuwa kumtafuta Peter kwa simu tuwekeane miadi ya kukutana. Nilitaka nikutane naye ana kwa ana ili tuweze kuzungumza mambo kadha wa kadha yaliyomhusu Fatuma. Nilijipa matumaini kwamba inawezekana angekuwa mtatuzi wa tatizo hilo nililokuwa nalo. Tulikubaliana kukutana nyumbani kwetu siku iliyofuata baada ya kumuelekeza jinsi angeweza kufika pale kiamboni. Siku hiyo ilipofika, Peter alifika pale nyumbani. Ilikuwa ni mwendo wa saa nane na vichopo hivi adhuhuri. Kila mmoja akafurahi ghaya kukutana na mwenzake madhali tulikuwa hatujapata kuonana baada ya muda mrefu tangu tulipoagana kule Uarabuni.

Tuliketi chini ya mti wa mkrismasi uliokuwa mkabala na nyumba ya wazazi wangu kwa ajili ya mazungu hayo huku tukinywa sharubati. "Karibu sana nyumbani kwetu ndugu Peter," nikamkaribisha Peter. "Ahsante sana ndugu Yohana," akashukuru Peter. "Pongezi kwa kuwajengea wazee wako jumba hili zuri." Peter akanihongera huku akinipa mkono wa tahania. "Nashukuru sana ndugu Peter. Wajua hawa wazazi

wetu huwa ni jambo la maana sana tukitia tabasamu kwenye nyuso zao wakiwa wangali hai hivi kwa wema wao. Hii ni njia mojawapo ya kutambua juhudi zao na kuwashukuru kwa malezi mazuri na elimu waliyonipa." Nikasema. "Naam! Ama kweli wanastahili shukrani maridhawa," akaongezea ndugu Peter. "Vipi kuhusu safari yako ya kuja nyumbani?" Peter akasaili. "Ahaa! Safari ilikuwa njema kabisa," nikajibu kwa bashasha. "Alhamdulilahi!" Akatamka Peter na kisha akauliza tena, "Vipi hali ya Tom Johnson na mkewe Bi. Huruma?" "Niliwaacha wakiwa wazima kabisa." Nikajibu. "Wabarikiwe sana wale malaika. Nawaita malaika kwa utu wao wa kuigwa." Akasema Peter. "Bila shaka! Watu kama hao hupatikana kwa tukizi mno." Nikasema kwa msisitizo.

Mazungumzo kati yetu wawili yaliendelea huku kila mmoja akiwa na shauku ya kujua yaliyomhusu mwenzake. "Hali ya shemeji vipi?" Peter aliuliza. Swali lake hilo likanifanya niwe kimya kwa kitambo kirefu kabla ya kulijibu. Ukimya huo ukamfanya Peter atambue kwamba lazima kulikuwa na tatizo. Nilishusha pumzi na kisha nikamjibu, "Sijui hali yake na hata aliko. Hii ilikuwa kati ya sababu ya kuomba kukutana nawe ndugu Peter." "Yani huwa hamzunguzi?" Peter akauliza kwa hamu kubwa ya kujua. "Naam. Huwa hatuzungumzi. Kila ninapomtafuta kwa simu hapatikani." Nikamwambia. "Pole sana ndugu Yohana. Kuna rafiki yake mmoja wa tangu zamani ambaye ninamfahamu. Yeye ni jirani yangu kule ninakoishi, naamini atatufaa mno katika hili. Wacha nitazungumza naye nione iwapo anajua lolote kumhusu Fatuma." Akasema Peter. "Nitashukuru sana," nikasema." Kupitia mazungumzo hayo, Peter alinifahamisha ya kwamba alikuwa amerudiana na mkewe huyo wa zamani aliyekuwa amemtalaki baada ya kujirudi na sasa walikuwa wakiishi pamoja. Habari hiyo ilinifurahisha mno. Baadaye tuliagana baada ya mazungumzo hayo marefu. Peter aliahidi kunifahamisha lolote atakalolibaini baada ya kuzungumza na rafiki yake.

Baada ya siku tatu hivi kupita, Peter alinipigia simu na kunifahamisha kuwa rafiki yake huyo alikuwa anajua alikoishi Fatuma na hata walikuwa wakiwasiliana na Fatuma mara kwa mara. Aidha, alikuwa amemuonyesha Peter sehemu hiyo alikoishi Fatuma. Peter alinifahamisha kuwa sehemu hiyo ilikuwa inajulikana kwa jina Ukwasini. Tayari nilikuwa ninaifahamu sehemu hiyo. Ilikuwa kiunga cha mji wa Mviringo kama nilivyoifahamu. Sehemu walikoishi matajiri tu. Hapo ndipo nilipotambua kuwa Fatuma alikuwa amegeuka sungura. Kumbe alikuwa kanichezea shere kwa kuniambia kuwa alikuwa amenunua shamba na kujenga nyumba kule Miinukoni. Niliweza pia kutambua kuwa alikuwa amenikatia mawasiliano kabisa na ndio maana kila nilipompigia simu hakuwa akipatikana hewani.

"Inawezekaje kuwa huwa anazungumza na sahibu yake mara kwa mara ilhali mimi nikimpigia simu huwa hapatikani hewani? Je, kwanini akaamua kunikatia mawasiliano licha ya mimi kuukabilisha moyo wangu kumtimizia kila alichokihitaji? Je, inawezekana aliamua kununua shamba na kujenga kule Ukwasini anakoishi? Lakini iwapo aliamua hivyo kwanini hakunihusisha katika hilo?" Nafsini nilijiuliza maswali haya kwa msururu bila kupata majibu yake. Maswali hayo yakawa fumbo lililokosa ufumbuzi wake wakati huo. Baadaye nilihisi kuwa ufumbuzi wa maswali hayo ungepatikana tu kwa njia moja. Njia yenyewe ilikuwa ni kwenda moja kwa moja hadi Ukwasini, kule alikokuwa akiishi, nikutane naye uso kwa macho. Baadaye Peter alinipa maelekezo ya kufika alikoishi Fatuma. Alinieleza mengi kuhusu eneo hilo alikoishi Fatuma ili kunirahisishia upatikanaji wake. Nilimpa Peter shukrani maridhawa kwa taarifa hizo na ushirikiano wake nami kwa kunifaa katika utatuzi wa tatizo hilo lililonipoka amani.

Maelekezo yake Peter yalikuwa dira iliyonielekeza hadi alikoishi Fatuma bila kupotea njia. Ama kweli sehemu hiyo ilikuwa ya wakwasi tu. Geti yenyewe ilijengwa kwa ustadi na ufundi wa hali ya juu.

Pale getini nilimkuta bawabu aliyevalia sare rasmi ya ulinzi katika boma hilo. Shati lake na chepeo aliyokuwa amevalia kichwani zote zilikuwa na nembo iliyoandikwa *Cobra Security Service*. Nilimuamkua kabla ya kumshitakia lililonipeleka mahala pale, "Habari yako ndugu," "Salama tu. Sijui nikusaidiaje?" Yule bawabu akajibu na kisha kuuliza. "Tafadhali naomba kumuona Fatuma."Nikamshitakia ombi langu. "Eti Fatuma? Hapa Hakuna mtu anayeitwa Fatuma."Yule bawabu akajibu. Jibu lake hilo likanishtua na kunitamausha mno. Nilipomuelezea kinagaubaga kuhusu maumbile yake akamtambua. "Aaaah! Haitwi Fatuma bali anaitwa Rita. Si unasema huyu mke wa mbunge wa eneo hili?" Bawabu yule akajibu na kisha kuniuliza. Ilinibidi ninyamaze kwa kitambo kidogo kabla ya kumjibu kutokana na hali ya kutokuwa na uhakika iwapo ni yule ambaye bawabu huyo alimtaja baada ya kumuelezea muonekano wa Fatuma. Alipoona nakawia kumjibu alisema, "Basi twende hadi pale mlangoni nikamuite ukamwone labda utamjua." "Nitashukuru sana ukimuita," nikajibu kwa bashasha ya kulazimisha huku tukifululiza naye hadi mlangoni.

Baada ya muda mfupi wa bawabu kubisha pale mlangoni kwa kubonyeza kitufe fulani pale mlangoni, mlango ulifunguliwa taratibu. Amini usiami aliyejitokeza alikuwa ni Fatuma macho yangu na yake yalipokutana. Alikuwa Fatuma mwenyewe kabisa. Nilishtuka zaidi ya nilivyowahi kushtuka maishani mwangu hasa nilipoona kuwa alikuwa na ujauzito baada ya yeye kujitokeza zaidi pale nje mlangoni. Naye alishtuka zaidi kuniona. Hakuamini kwamba ningeweza kujua hapo alipokuwa akiishi. Ugoigoi wa kutembea huku akijishika kiunoni ulidhihirisha jinsi ujauzito huo ulikuwa umemchosha vya kutosha. Kumbe Fatuma alikuwa amebadilisha jina lake. Sikuamini kilichokuwa kimetokea kabisa. Nilijaribu kutamka hata herufi moja tu ya neno nikashindwa. Nilitekewa. Kwa ghadhabu na mshtuko mkubwa akanifokea, "Huyu nani tena? Ondoka hapa mara moja au nikuitie polisi sahizi!" "Wewe kwanini umekifungulia kinyesi hiki geti? Hata kinanitia kichefuchefu!" Fatuma akamfokea

bawabu yule huku akijipepea kwa vidole vyake vyenye kucha ndefu. "Fatuma mke wangu, una..." Nikajaribu kuzungumza ila nikakatizwa na Fatuma, "Eti nini? Hivi hujui kuwa fimbo ya mbali haiui nyoka? Mkataba wangu nawe uliisha kitambo sana, nililimatia tu kukutaarifu. Ondoka!" Baada ya muda mfupi bwana mmoja mwenye umri sawa na wa baba yangu kwa muonekano wake alikuja hapo mlangoni toka chumbani. "Kuna nini *honey. What is not happening my wife?"* Kauli yake bwana yule ilinidhihirishia uhusiano wake na Fatuma. Kumbe walikuwa mume na mke na tayari walikuwa wanatarajia kikembe.

Nilibaki nimeachama tu huku nikiumbuliwa na kudhalilika mbele ya wapenzi hao. "Mume wangu ni hili jitu linalodai kwamba mimi ni mke wake ilhali hata sijawahi kuliona." Fatuma akamjibu yule bwana. "Aaah! Kijitu hiki tu? Wewe kijana hebu ondoa takataka hii hapa mara moja kabla sijaifyatua risasi!" Yule bwana akamuamrisha bawabu. Baadaye bwana yule akaanza kumgusagusa Fatuma tumbo lake hilo lililokuwa limejitokeza zaidi kutokana na ujauzito wake na kumbusu pia shavuni huku akimpembeja mbele ya macho yangu. Sikuamini macho yangu kabisa. Nilidhani nilikuwa ndotoni ninakabiliwa na jinamizi lililoelekea kuniangamiza. Kipindi hicho chote macho yalikuwa yamenitoka pima huku mdomo wangu ukiwa wazi kabisa kwa mtamauko huo ambao sidhani kama kulikuwa na mfano wake popote pale. Kuendelea kuona maumbufu hayo kukawa zaidi ya uwezo wangu. Nilijidondokea chini pu! kama gunia la viazi nikazirai kabla ya bawabu yule kunifikia. Kilichotokea hatimaye sikukijua.

Hospitalini kwenye kitanda ndiko nilikojikuta baadaye baada ya fahamu kunirudia. Kumbe ndiyo iliyokuwa athari ya mtamauko wa yaliyonikuta siku hiyo. Nilishtuka mno kujikuta katika mazingira hayo yaliyotawaliwa na ukimya pamwe na harufu kali za dawa mbalimbali. Pale kitandani nilijitahidi kuangazaangaza macho yangu hapa na pale.

Nikawaona wazazi wangu wote wawili na Peter wakiwa wamenizingira pale kitandani. Waliniangalia kwa imani kubwa mno. Uso wake mama ulioshamiri mavune ulidhihirisha uchungu uliomkabili kwa shuruti. Alikuwa amelia hadi machozi yenyewe yakasita kumtoka machoni. Yumkini angeendelea kulia basi angelia damu.

Jinsi nilivyojikuta pale hospitalini ilikuwa fumbo nililoshindwa kulifumbua kwa siku ayami hadi nilipohadithiwa na Peter ***nususi hiyo ya mambo***. Awali sikuwa na taarifa yoyote kuhusu yaliyotokea baadaye. Nilichoweza kukumbuka tu ni kwamba nilikumbwa na mtamauko baada ya kukutana na Fatuma. Peter aliniambia kwamba niliokotwa asubuhi barabarani karibu na alikoishi Fatuma na wasamaria wema ambao walinikimbiza hospitalini. Mwanzoni walidhani nilikuwa nimekwishatangulia mbele za haki. Hapo ndipo nilipopata mwanga kamili wa jinsi nilijikuta katika mazingira hayo ya hospitalini. Kumbe baada ya kuzirai kwangu siku hiyo na jioni hiyo ya mtamauko, Fatuma alimshauri yule 'mume wake' kuwa ingekuwa bora wanitupe barabarani, wasije wakalimbikiziwa lawama ya mauaji. Wapenzi hao walidhani ya kwamba nilikuwa nimekata roho baada ya kuona kwamba sikuwa ninapumua wala kufurukuta. Jambo ambalo walilifanikisha kwa kuwakomboa watu walionibeba hobela hobela wakanitupa barabarani kwenye mtaro ambao ulikuwa ukiyaelekeza maji chafu katika sehemu husika. Kumbe usiku kucha nilipiga mbizi katika maji hayo chafu. Kusadiki kwamba Fatuma angeweza kunitendea uhayawani huo ulikuwa ni zaidi ya uwezo wangu. Sikuweza kabisa!

# *Sura ya kumi na tatu*

Niliruhusiwa kwenda nyumbani baada ya hali yangu ya afya kuimarika hatimaye. Baada ya miezi mitatu ya kuwaza na kuwazua cha kumfanyia Fatuma, nilifikia uamuzi niliohisi kwamba ulikuwa sahihi kabisa. Hasira za mkizi nilizokuwa nazo sasa zilikuwa zimeisha kabisa. Moyoni mwangu hamkuwepo na hata chembechembe pekee za kinyongo dhidi yake Fatuma. Uamuzi wenyewe ulikuwa ni kuukabilisha moyo wangu kumsamehe Fatuma kwa yote aliyonitendea kupitia waraka huu niliomwandikia:

*Kwa Fatuma,*

*Hujambo hapo ulipo Fatuma? Mimi nilipo sijambo. Madhumuni ya kukuandikia waraka huu ni kukuarifu kwamba sina kinyongo nawe hata baada ya kunitamausha kwa kunitendea uliyonitendea. Uliyonitendea haikustahili kabisa kuwa malipo ya wema wote niliokutendea na mapenzi ya dhati niliyokuwa nayo kwako. Haikustahili kabisa, ninasisitiza! Haijaniwia rahisi kuamini hayo yote. Siku zote nimekuwa nikidhani kwamba nimo ndotoni ninakumbana na jinamizi hatari linalotaka kunipoka pumzi ila sasa imenibidi nikubali kwamba niliyokumbana nayo yalikuwa katika ulimwengu halisi na wala si ndotoni tena. Ama kweli ulibadilika baada ya kubadilisha jina na tabia! Ninasikia kwamba siku hizi unaitwa Riziki, tena mke wa mbunge wa eneo la Ukwasini. Fatuma jina lako la mwanzoni lililobeba mapenzi ya dhati kwangu na utu si lako tena. Maaja kweli! Chanzo cha kubadilika kwako kwangu ni usiku wa kiza totoro. Si neno madhali hata nikijua sasa hakitanifaidi kwa lolote wala chochote zaidi ya kunirefushia tu vya kusimuliwa katika historia yangu. Kitumbua kimekwishaingia mchanga. Hakiliki tena! Tambua kwamba kati ya kulipiza kisasi na kukusamehe nimechagua kukusamehe. Hili ndilo chaguo ninaloliona bora zaidi. Hela zote nilizokuwa nikikutumia*

*ninakuwachia uzitumie kwa manufaa yako na familia yako ila kuwa makini sana madhali dunia imejaa hadaa. Kwaheri!*

*Mchumba wako wa awali,*

*Mstahimilivu Yohana.*

Sikuwahi pokea ujumbe wowote wa kuniomba msamaha wala wa kunishukuru kwa msamaha wangu huo toka kwa Fatuma licha ya kumwandika waraka huo. Mara kwa mara alikinitumia jumbe za vitisho na dharau tu kwa njia ya simu hadi nilipoamua kudhibiti namba yake hiyo na kuifuta kabisa kwenye simu yangu ili nisipokee jumbe hizo tena. Kupitia jumbe hizo, alijinaki pia jinsi mumewe huyo alikuwa na uwezo wa kunifanyia lolote madhali alikuwa mbunge. Sikuwa na budi kuwapisha hao waliojiona wenye nguvu zaidi. Malipo kwa aliyonifanyia nilimwachia Mungu huku nikitambua kwamba dunia siku zote ni duara.

* * * *

Muda mrefu umepita tangu nilipokumbwa na mtamauko huo. Funzo alilonipa Fatuma limenifanya niishi kwa tahadhari mno. Kwa sasa simuamini mtu yeyote yule kirahisirahisi tu. Nilishaumwa na nyoka na sasa kila niuonapo ung'ong'o mimi hushtuka. Hata mke wangu Neema nimechukua muda mrefu sana kuanza kumuamini na bado ninaendelea kuujenga msingi huo wa kumuamini zaidi. Haikuniwia rahisi kuridhia kuishi naye kama mke wangu wa ndoa hadi wazee wangu walipoingilia kati na kunihimiza nimuoe. Fatuma alikuwa amenivunja moyo kabisa wa kupenda tena na kumuamini mwanamke baada ya kunitendea uhayawani huo. Awali nilishikilia kuwa wanawake wote ni sawa tu lakini baadaye niligundua kuwa kumbe si hivyo. Hawako sawa hata kidogo hasa kitabia.

Sasa ninatambua kuwa kitabia, kuna kategoria mbili ya wanawake na wanaume vilevile. Kadhalika ninatambua kwamba tabia inaweza kuwa

kigezo kinachoweza kutumiwa kubainisha aina za watu; watu wazuri na wabaya. Watu wanaweza kuwekwa katika kategoria mbili kitabia; kategoria ya kwanza ni ya wale ambao huufikicha ubaya wao na kuudhihirisha baadaye baada ya kupata walivyokuwa wakivimezea mate kama alivyokuwa Fatuma. Mwanzoni hawa hujifanya wazuri kabisa hadi wapatapo hivyo wavitakavyo kwa mtu. Wametawaliwa na tamaa tu. Kategoria ya pili ni ya wale ambao huufichua uzuri wao siku zote na kuudumisha daima dawamu bila kuyumbishwa na misukumo wala vishawishi vya maisha. Aidha, wao huweka wazi udhaifu na ubaya wao siku zote na huwa tayari kurekebika pindi wanaporekebishwa. Sasa baada ya tathmini zangu za muda mrefu najua pa kumuweka Neema mke wangu. Ninamuweka katika kategoria hii ya pili. Hapa ndipo afaapo kabisa.

Neema alirudi nchini toka Uarabuni baada ya ubaguzi dhidi ya Waafrika kukithiri kule. Dhuluma za aina mbalimbali na vifo vya Waafrika vilivyojengwa kwa msingi wa ubaguzi wa rangi na asili Uarabuni ndivyo vilivyokuwa vichwa vya vyombo vingi vya habari. Kutokana na hali hiyo serikali ilichukua hatua ya kuwakwamua Wanahawinde toka katika hatari hiyo kwa kuwarejesha nchini ili kuondokana na dhuluma zaidi dhidi yao.

Mimi na mke wangu Neema tulishapata kazi humu nchini mwetu Hawinde. Mimi ni mhandisi mkuu katika kampuni ya *Tujenge Company* na mke wangu Neema ni mhasibu katika benki kuu ya taifa. Tunaishi Miinukoni ambako tumejijengea jumba la kifahari ambalo kila anayeliona hakosi kulihusudu kwa mvuto na mnato wake wa kupigiwa mfano. Ama kweli limejengwa kwa ufundi na ustadi wa kiwango cha juu. Mimi mwenyewe ndiye niliyechora ramani yake na kushauri mkao na mtindo wake.

Ni majira ya saa nane adhuhuri. Jua bado linawaka kama kwamba linataka kuviteketeza vitu vyote ardhini. Tumeukwepa udhalimu huu wa jua kwa kuamua kujipumzisha barazani huku tukinywa sharubati ya

maembe; mimi na mke wangu Neema. Katika kujipumzisha huku, tunahadithiana na kusimuliana mengi ya Uarabuni. Ikiwemo ya kufurahisha na ya kuhuzunisha. Mara tunashtuliwa na ujio wa Tunu mwanetu anayefika huku akihemahema. "Kuna nini mwanangu?" Anauliza mamake Kisha Tunu anajibu, "Ba...Baba! Kuna mgeni anayeomba kukuona pale getini." "Sawa mwanangu. Mwambie naja sasa hivi." Ninamwambia Tunu ambaye anatoka mbio mara moja akielekea getini. Ninajinyanyua hapa kochini na pindi ninapoanza kwenda ninasita kidogo na kujiuliza, "Ni nani huyu anayeomba kuniona na ana nini la kuniambia, au ni Peter? Naam, inawezekana ni Peter." "Wewe nenda ukaone ni nani," ananiambia Neema huku naye akijinyanyua pale kochini na kuelekea jikoni. "Sawa, wacha nikamuone." Nikasema na kuondoka.

Baada ya kufungua geti tu hivi, ninapigwa na butwaa kumuona Fatuma. Kasawijika vya kumtosha kama ninavyomuona. Kilichomfika ndicho sikijui na wala sitaki kukijua. Ananiangukia magotini na kuanza kwikwi zake, "Yo...Yoha...na... Yohana..." Sina muda wa kumsikiliza kabisa madhali kama ni kumsamehe nilikwishamsamehe miaka mingi iliyopita. Ninamjibu tu kwa maneno mawili, "Nilishakusamehe Fatuma!" Hatimaye ninajiondokea baada ya kufunga geti na kumwacha hapo akijililia kama mtoto mdogo aliyenyimwa pipi. Bora nirudi ndani niendelee na shughuli zangu.

# ***Sherehe***

**A**

**Amilifu...............** hai na changamfu.

**Adibu.................**-enye adabu au heshima.

**Akamtalaki.........**Akamwacha/ akasitisha uhusiano wa ndoa.

**Alilimbika...........**Aliweka ili ziwe nyingi.

**F**

**Faradhi.............**Lazima

**H**

**Hadhi................** Heshima

**Hadubini............**Chombo kinachovifanya vitu vilivyo mbali au vidogo zadi vionekane

vizuri

**Halingenifutu......**Halingenipita hasa katika kulisikia.

**Hamtelekezi........**Hamwachi.

**I**

**Itengemae .........**Iwe nzuri pia itengenee.

**K**

**Kajifunga masombo.........**Kajitahidi zaidi; kujifunga kiwewe.

**Kuwatelekeza....................**Kumwacha kuwashughulikia au kuwacha kuwajalia.

**Kumpiku..........................**Kumzidi au kumshinda kwa jambo.

**Kufu................................** Hali kuendana katika kiwango.

**Kusuudika .....................**Kubahatika/ kuneemeka.

**Kunafasika.....................**Kupata ufanisi au mafanikio.

**Kuitehemu.....................**Kuivunjia heshima/ kuishishia hadhi.

**Kuuvuaza.......................**Kukosesha utulivu hasa wa moyo/ kuvuruga moyo.

**Karandinga....................**Gari hasa la askari ambalo hutumiwa kubeba wahalifu.

**M**

**Mchuuzi.......................**mtu anayeuza bidhaa ndogondogo hasa kwa kivitembezatembeza kwa watu mijini.

**Mashangingi...............** Magari ya kifahari.

**Maashiki....................**Wenye mapenzi makubwa kwa kitu au Jambo fulani.

**Makuruhu...................**Mambo yasumbuayo.

**Masimbi.....................**Masalio ya buzaa.

**Maumbufu..................**Mambo ya kumuumbua mtu au kumdhalilisha.

**Mashuzi....................** Maganda ya ndizi ambayo hayana thamani.

**Mwao........................**Habari kuhusu Jambo.

**N**

**Nakama.....................**Matokeo mabaya.

**Nikapiga bismilahi.........**Nikamuomba Mungu/ Nikasali.

**Nyoyo kubwa.............** Karimu/ -enye kusaidia.

**Nususi ya mambo.......**Uwazi wa mambo.

**Nyota ya jaha...............**Bahati njema.

**S**

**Sikuyatelekeza...........**Sikuwacha kuyawajibikia.

**Simu fifi.............**Wito wa simu ambao haujapokelewa.

**Tukizi.................**Vigumu kutokea au kuonekana, pia nadra.

**Tumepezana.......**Tumekosa kuonana baada ya muda mrefu.

**U**

**Ukata.................**Umaskini; Ufukara au uhawinde.

**Ukalili................**Ukosefu pia uchechefu.

**Umfutu............**Umpite

**Usono.............**Usingizi.

**Ukamfaradhisha.............**Ukamlazimu.

**Ufanifu.............................**Mafanikio au ufanisi.

**Ubahaimu........................**Hali ya kumtendea binadamu mwenzio mambo yasiyofaa/

Unyama.

**Usahali............................**Wepesi au urahisi wa kufanya jambo.

**Utatamauka....................**Utapatwa na mshtuko hasa kwa jambo lililokinyume na

matarajio yako.

**W**

**Wakwasi......................**Matajiri; wenye navyo.

**Wanajikusuru.............**Wanajinyima kwa nia fulani.

**Wanatunyanyapaa.......**Wanatuepuka.

**Wakijitutumua.............**Wakijitahidi zaidi.

**Z**

**Zimemuelemea...........**Zimemshinda kwa nguvu au uwezo/ zimemzidia.

**Zani................**Vurugu.

*(Ilikamilishwa 23 Agosti 2023 saa nane)*